**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

# WIZARA YA AFYA ZANZIBAR

**HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA**

**MHE. NASSOR AHMED MAZRUI**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI**

**KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

***Mei, 2025***

# WIZARA YA AFYA - ZANZIBAR



***Mhe. Nassor Ahmed Mazrui***
***Waziri wa Afya***
***Zanzibar***



***Mhe. Hassan Khamis Hafidh***
***Naibu Waziri wa Afya***
***Zanzibar***



***Dkt. Mngereza Mzee Miraji***
***Katibu Mkuu***
***Wizara ya Afya***
***Zanzbiar***



***Dkt. Amour S. Mohamed***
***Mkurugenzi Mkuu***
***Wizara ya Afya***
***Zanzbiar***

**YALIYOMO**


| *Mada* | *Ukurasa* |
|---|---|
| **MCHANGANUO WA VIFUPISHO** .......................................... | **iii** |
| **A. UTANGULIZI** .......................................... | **1** |
| **B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25**.................... | 7 |
| *o* ***MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025***................. | ***9*** |
| **UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA** ***.......................................*** | ***11*** |
| ***PROGRAM YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101)***.............................. | ***13*** |
| o **HUDUMA ZA MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI, HOMA YA INI, KIFUA KIKUU NA UKOMA** .......................................... | **13** |
| o **HUDUMA ZA KUMALIZA MALARIA ZANZIBAR** .......................................... | **18** |
| o **HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI, MAMA NA MTOTO** .......................................... | **20** |
| *o* ***HUDUMA ZA MARADHI YASIYOAMBUKIZA*** .......................................... | ***22*** |
| o ***HUDUMA YA UFUATILIAJI WA MIENENDO YA MARADHI*** .......................................... | **23** |
| *o* ***HUDUMA ZA MARADHI YASIYOPEWA KIPAUMBELE*** .......................................... | ***24*** |
| o ***HUDUMA ZA MSINGI ZA MATIBABU YA MACHO .......................................*** | **25** |
| *o* ***HUDUMA YA UTOAJI WA ELIMU YA AFYA NA URATIBU WA WAHUDUMU WA AFYA NGAZI YA JAMII .......................................*** | ***26*** |
| o **HUDUMA ZA AFYA NGAZI YA JAMII** .......................................... | 27 |
| *o* ***HUDUMA ZA AFYA YA MAZINGIRA*** .......................................... | ***28*** |
| *o* ***HUDUMA ZA AFYA BANDARINI NA VIWANJA VYA NDEGE*** .......................................... | ***29*** |
| *o* ***HUDUMA YA AFYA YA WAFANYAKAZI*** .......................................... | ***30*** |
| *o* ***HUDUMA ZA AFYA YA MSINGI YA AKILI*** .......................................... | ***31*** |
| **UTEKELEZAJI WA BODI NA MABARAZA YA TAALUMA ZA AFYA** .......................................... | **32** |
| o **BARAZA LA TAALUMA ZA AFYA YA JAMII NA MAZINGIRA** .......................................... | **32** |
| **PROGRAMU YA HUDUMA ZA TIBA (PH0102)** .......................................... | ***32*** |
| *o* ***PROGRAM NDOGO YA HUDUMA ZA MATIBABU*** .......................................... | ***34*** |
| *o* ***HUDUMA ZA UCHUNGUZI*** .......................................... | ***35*** |
| *o* ***HUDUMA ZA USHIRIKIANO WA AFYA KIMATAIFA*** .......................................... | ***35*** |
| *o* ***HUDUMA ZA DAMU SALAMA*** .......................................... | ***36*** |
| *o* ***HUDUMA ZA MKONO KWA MKONO (ONE STOP CENTRE)*** .......................................... | ***36*** |
| *o* ***HUDUMA ZA BODI NA MABARAZA YA TAALUMA ZA AFYA*** .......................................... | ***37*** |
| *o* ***BODI YA USHAURI YA HOSPITALI BINAFSI*** .......................................... | ***37*** |
| *o* ***BARAZA LA TIBA ASILI NA TIBA MBADALA*** .......................................... | ***38*** |
| *o* ***BARAZA LA MADAKTARI*** .......................................... | ***39*** |
| *o* ***BARAZA LA WAUGUZI NA UKUNGA*** .......................................... | ***39*** |
| *o* ***BARAZA LA WATAALAMU WA MAABARA ZA TIBA*** .......................................... | ***40*** |
| *o* ***HUDUMA ZA UUGUZI NA UKUNGA*** .......................................... | 40 |
| **HUDUMA YA UPATIKANAJI, UHIFADHI, USAMBAZAJI WA DAWA NA VIFAA TIBA** .......................................... | **41** |

| *Mada* | | *Ukurasa* |
|---|---|---|


- o *OFISI YA MFAMASIA MKUU WA SERIKALI* ................................................ ***41***
- o ***WAKALA WA BOHARI KUU YA DAWA*** ..................................................... **42**

**PROGARAMU NDOGO YA HUDUMA ZA UCHUNGUZI (SH030202)** ................ **43**

- o ***WAKALA WA CHAKULA DAWA NA VIPODOZI*** ......................................... ***43***
- o ***WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI*** ...................... **44**

**PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0103)** ................ 45

- o ***PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI (SH010301)*** ........... **47**
  - ***NGUVU KAZI YA SEKTA YA AFYA*** .............. ***48***
  - ***HUDUMA ZA UNUNUZI NA UONDOAJI WA MALI ZA UMMA*** ............. ***49***
- o ***HUDUMA ZA AFYA KIDIGITALI*** .............. *49*
- o ***PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI (SH010302)*** ........... 50
  - **MIRADI YA MAENDELEO** ...................................................................... 53
  - **MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR (ZHSF)** ............................. **56**
  - ***TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZA BINAADAMU (ZAHRI)*** ..................... ***58***
- o **PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA WIZARA YA AFYA PEMBA (SH010303)** ........................................................................ **59**
- o **PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (FUNGU H02)** .................... 60

**C. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025** ........... **64**

**HATUA ZA UTATUZI WA CHANGAMOTO** ......................................................... **65**

**D. MWELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26** ............................................................................... ***67***

- **o** ***RASILIMALI WATU KWA SEKTA YA AFYA*** ................................................... ***68***
- **o** ***KUGHARAMIA HUDUMA ZA AFYA*** ............................................................. 69
- **o** ***MIUNDOMBINU YA AFYA NA UPATIKANAJI WA DAWA NA VIFAA TIBA*** ... *69*
- **o** ***UPATIKANAJI WA TAARIFA ZA AFYA*** ........................................................ ***69***
- **o** ***UONGOZI NA UTAWALA WA SEKTA YA AFYA*** .......................................... ***69***
- o ***PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101)*** ............................... ***72***
- o ***PROGRAMU YA TIBA (PH0102)*** .................................................................. ***73***
- o ***PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA AFYA (PHO103)*** ***74***

**PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA FUNGU (H02)** .......................... **75**

**E. SHUKURANI** .................................................................................................. **77**

**F. HITIMISHO** .................................................................................................. **79**

- o ***MAOMBI YA FEDHA KWA UTEKELEZAJI WA KAZI ZILIZOPANGWA KWA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026*** ............. ***79***
- o ***MAPATO*** .................................................................................................. ***79***
- o **MATUMIZI YA KAWAIDA** ................................................................................ **79**

## MAELEZO YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| AMREF | - | Africa Medical Research Foundation |
| ARV | - | Anti-Retroviral Virus |
| BADEA | - | Arab Bank for Economic Development in Africa |
| BOQ | - | Bill of Quantities |
| CBM | - | Christian Blind Mission |
| CDC | - | Centre for Disease Control and Prevention |
| CPAP | - | Continuous Positive Airway Pressure |
| CT scan | - | Computed Tomography |
| CHV | - | Community Health Volunteers |
| CHW | - | Community Health Workers |
| CRDB | - | CRDB Bank |
| DFID | - | Department for International Development |
| EAC | - | East African Community |
| EMR | - | Electronic Medical Records |
| ENT | - | Ear Nose and through |
| eLMIS | - | Electronic Logistic Management Information System |
| GCP | - | Google Cloud Platform Services |
| GFATM | - | Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis and Malaria |
| GIZ | - | German Agency for International Cooperation |
| HIPZ | - | Health Improvement Project Zanzibar |
| HPV2 | - | Human papillomavirus types 2 (HPV-2) |
| IHI | - | Ifakara Health Institute |
| ICU | - | Intensive Care Unit |
| JICA | - | Japan International Cooperation Agency |
| JKCI | - | Jakaya Kikwete Cardiac Institute |
| KFD | - | Kyasanur forest disease |
| KMKM | - | Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar |
| KCMC | - | Kilimanjaro Christian Medical Centre |
| LAD | - | Large Anonymous Donor |
| MBLW | - | Mjumbe wa Baraza La Wawakilishi |
| MDH | - | Management and Development for Health (MDH) |
| MIOT | - | Madras Institute of Orthopedics’ and Traumatology |
| MNAP | - | Multi-sectoral Nutrition Action Plan |
| MOI | - | Muhimbili Orthopaedic Institute (MOI) |
| MP-AES | - | Microwave Plasma Atomic Emission Spectoscopy |
| MRI | - | Magnetic Resonance Imaging |

| | | |
|---|---|---|
| NHIF | - | National Health Insurance Fund |
| NBC | - | National Bank of Commerce |
| PBZ | - | People Bank of Zanzibar |
| PDB | - | Presidental Delivery Bureau |
| PENTA | - | Pentavalent vaccine |
| PEPFAR | - | The U.S. President’s Emergency Plan for AIDS Relief |
| PMI | - | President’s Malaria Initiatives |
| PPH | - | Postpartum Hemorrhage |
| SFD | - | Sorsby Fundus Dystrophy |
| SMT | - | Surface-Mount Technology |
| SMZ | - | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| TASAF | - | Tanzania Social Action Fund |
| TEHAMA | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| THPS | - | Tanzania Health Promotion Support |
| TOTs | - | Training of Trainers |
| TTCL | - | Tanzania Telecommunication Company Limited |
| U.A.E | - | United Arab Emirates |
| UAT | - | User Acceptance Testing |
| UKIMWI | - | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| UNAIDS | - | United Nations Programme on HIV/AIDS |
| UNDP | - | United Nations Development Program |
| UNFPA | - | United Nations Population Fund |
| UNICEF | - | United Nations International Children Fund |
| USAID | - | United States Agency for International Development |
| UVKO-19 | - | Ugonjwa wa Virusi vya Korona - 19 |
| VVU | - | Virusi Vya UKIMWI |
| WHO | - | World Health Organization |
| YFS | - | Youth friendly services |
| ZADEP | - | Zanzibar Development Plan |
| ZAHRI | - | Zanzibar Health Research Institute |
| ZanLIS | - | Zanzibar Laboratory Information System |
| ZBC | - | Zanzibar Broadcasting Cooperation Television |
| ZCTV | - | Zanzibar Cable Television |
| ZFDA | - | Zanzibar Food and Drug Agency |
| ZHSF | - | Zanzibar Health Services Fund |
| ZOP | - | Zanzibar Outreach Program |
| ZSSF | - | Zanzibar Social Security Fund |

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi ambayo imepitia na kuchambua kwa kina bajeti ya Wizara ya Afya, naomba kutoa hoja kwamba sasa Baraza likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2024/25 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2025/26. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2025/26.

2. **Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu na kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, kwa kipekee naomba kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** kwa kuendelea kuniamini kusimamia Wizara ya Afya ambayo ndiyo yenye dhamana ya kusimamia masuala ya Afya nchini. Sekta hii inagusa maisha ya kila mwananchi kutokana na ukweli kuwa bila ya Afya hakuna maendeleo.

   Vilevile, nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuipa kipaumbele Sekta hii kwa kutoa miongozo, maelekezo mbalimbali na kufanya uwekezaji mkubwa wa rasilimali fedha ili kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya

kwa wananchi. Aidha, niwapongeze **Mheshimiwa Othman Masoud Othman** Makamo wa Kwanza wa Rais na **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla** Makamo wa Pili wa Rais kwa mashirikiano mazuri wanayompatia Mheshimiwa Rais katika kuiongoza nchi yetu. Vilevile, nachukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi **Mhandisi Zena Ahmed Said** kwa ushauri na maelekezo anayotupatia katika kuleta ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za wizara.

3. **Mheshimiwa Spika,** Nichukuwe fursa hii kukupongeza wewe binafsi, kwa kuendelea kuliongoza Baraza hili kwa umakini kabisa. Pia nawapongeza Naibu Spika, **Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma**, Wenyeviti wa Baraza na Kamati za Kudumu na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa namna wanavyotoa hoja na michango inayopelekea kuleta ufanisi na uwajibikaji wa watendaji wa taasisi mbali mbali na kurahisisha maendeleo. Napenda kukuhakikishia kuwa uongozi wa Wizara ya Afya utaendelea kusimamia utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo, ushauri na maelekezo yanayotolewa na Baraza lako tukufu namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekima, busara na umakini.

4. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii inayoongozwa na **Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani** Mwakilishi wa Viti Maalum, kwa ushauri na maelekezo

wanayoyatoa yenye lengo la kuimarisha huduma za afya nchini hususan wakati wanapofanya ziara katika Wizara na Taasisi zake. Ninawaahidi waheshimiwa wajumbe kuwa Wizara yangu itaendelea kuzingatia ushauri na mapendekezo yenu katika kutekeleza majukumu yetu kwa wananchi.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutambua mambo makubwa yaliyofanywa na **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** katika sekta ya afya kwa kipindi cha miaka minne ya uongozi wake kama ifuatavyo:-

   a. Kukamilika kwa ujenzi na kuanza utoaji wa huduma kwenye hospitali **10** za Wilaya (Unguja ni Ijitimai, Chumbuni, Mbuzini, Mwera Pongwe, Kitogani, Pangatupu na Kivunge na Pemba ni Micheweni, Kinyasini na Vitongoji) na moja ya Mkoa –Lumumba;

   b. Kukamilika kwa ujenzi wa nyumba za makaazi ya wafanyakazi zinazo hudumia familia **76** katika Hospitali ya Rufaa ya Abdalla Mzee-Mkoani Pemba pamoja na kufikia hatua za mwisho za ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali za Wilaya Mwera Pongwe, Kitogani na Pangatupu kwa Unguja na kwa upande wa Pemba katika hospitali ya Kinyasini na Vitongoji;

   c. Kukamilika kwa mitambo **3** ya kuzalisha hewa tiba katika hospitali za Wilaya Mwera Pongwe, Vitongoji na Hospitali ya Mkoa Lumumba na kuanza uzalishaji wa hewa tiba ambapo kwa siku jumla ya mitungi **350** yenye ujazo wa lita **50** huzalishwa;

d. Kuongezeka kwa Vifaa tiba vya kisasa vya uchunguzi na ugunduzi wa magonjwa mbali mbali ikiwemo;- MRI kutoka **1** hadi **2**, CT-Scan kutoka **2** hadi **3**, Digital X-Ray kutoka **3** hadi **19**, Ultrasound kutoka **10** hadi **34**, Echocardiogram (ECO) kutoka **1** hadi **3**, Electocardiogram(ECG) kutoka **4** hadi **12**, Mamogram **1**, Dialysis mashine kutoka **10** hadi **32;**

e. Kukamilika kwa ujenzi wa Tanuri mbili kubwa (High Tech Incinerators) za kuchoma taka za Hospitali, Kibele kwa Unguja yenye uwezo wa kuchoma kilogramu **900** kwa saa na kwa upande wa Vitongoji kwa Pemba ina uwezo wa kuchoma kilogramu **750** kwa saa;

f. Kuongezeka kwa hospitali zinazotoa huduma za tiba za dharura kutoka hospitali mbili (**2)** mwaka 2020 hadi kufikia hospitali **15** kwa mwaka 2025;

g. Kuimarika kwa huduma za wagonjwa mahututi kwa kuongeza maeneo ya kutoa huduma hiyo kutoka hospitali moja (**1**) kwa mwaka 2020 hadi kufikia hospitali **16** kwa mwaka 2025;

h. Kuongezeka kwa gari za kubeba wagonjwa (Ambulances) kutoka **10** kwa mwaka 2020 kufikia **26** kwa mwaka 2025;

i. Kuongezeka kwa boti za kubeba wagonjwa (Ambulance Boat) kutoka **1** mwaka 2023 hadi kufikia **6** kwa mwaka 2025;

j. Kununua gari **5** za kutoa huduma za Kliniki tembezi (Mobile Clinics) kwa mwaka 2025;

k. Kupungua kwa vifo vya akinamama vinavyotokana na uzazi kutoka vifo **166** kwa mwaka 2020 hadi kufikia vifo **119** kwa mwaka 2024 kwa kila vizazi hai **100,000**;

l. Kuanza kutoa huduma za kibingwa za upasuaji wa Nyonga na Magoti bandia "Knee and Hip Replacement" katika Hospitali ya rufaa ya Mkoa Lumumba;

m. Kuimarika kwa huduma ya afya ya akili kwa kuongezeka kwa vituo vinavyotoa huduma ya afya ya akili kutoka vituo vya afya **34** kwa mwaka 2023/2024 kufikia vituo **55** kwa mwaka 2024/2025;

n. Kuifanya Bohari Kuu ya Dawa kuwa Wakala na kuipa mamlaka ya kununua, kuuza, kutengeneza, kuhifadhi na kusambaza dawa na vifaa tiba sambamba na kuingia mikataba na wazalishaji wa dawa ndani na nje ya nchi;

o. Upatikanaji wa dawa muhimu nchini umeimarika kutoka asilimia **63** kwa mwaka 2022/2023 kufikia asilimia **95** kwa Hospitali na asilimia **86** kwa upande wa Vituo vya afya kwa mwaka 2025;

p. Kuimarika kwa mifumo ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia huduma za afya ikiwemo kuanzishwa na kuanza kazi kwa Mfuko wa huduma za afya Zanzibar (ZHSF) na kuimarisha mashirikiano na sekta Binafsi;

q. Kuanza kazi kwa Maabara mpya ya kisasa ya Wakala wa Chakula na Dawa Zanzibar;

r. Kurasimishwa kwa kada ya wahudumu wa afya ya jamii na kuanzishwa kitengo maalumu cha kusimamia shughuli za watoa huduma za afya wa ngazi ya jamii;

s. Kuongeza idadi ya watumishi walioajiriwa kutoka watumishi wa afya **559** kwa mwaka 2020/2021 hadi kufikia wapya **2,008** wa kada mbalimbali ikiwemo madaktari **487**, wauguzi **892** na wafamasia **260** kwa mwaka 2023/2024; na

t. Huduma za Afya katika ngazi ya hospitali zinatolewa kwa kutumia mifumo ya TEHAMA katika maeneo yote ya utoaji wa huduma.

6. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kutoa maelezo ya awali, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2024/25, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na maombi ya fedha ya kutekeleza vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2025/26.

## B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

7. **Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2050), Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (2021/22 – 2025/26), Sera ya Afya ya Mwaka 2011 ambayo imeshafanyiwa mapitio mwaka 2025, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2020-2025, Mpango Mkakati wa Nne wa Sekta ya Afya - HSSP IV (2020/21 – 2024/25), Maagizo ya Serikali pamoja na makubaliano ya Kikanda na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

8. **Mheshimiwa Spika,** Katika bajeti ya mwaka 2024/25, Wizara kwa kushirikiana na Wadau mbali mbali zikiwemo Taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali na Washirika wa Maendeleo ilipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

   a. Kuimarisha miundombinu ya afya katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya ikiwemo matengenezo ya majengo na vyombo vya usafiri;

   b. Kuhakikisha upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na vitendanishi;

   c. Kuimarisha mifumo ya kidigitali ya taarifa za afya;

   d. Kuimarisha ubora wa utoaji wa huduma za afya kwa kuajiri wataalamu wenye sifa na kupeleka masomoni madaktari na wafanyakazi wa kada nyengine za afya;

e. Kuimarisha mifumo endelevu ya kugharamia huduma za afya ikiwemo Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar;

f. Kuimarisha huduma za afya ya msingi kupitia wahudumu wa afya ngazi ya jamii;

g. Kupunguza vifo vya mama wajawazito kutoka vifo **145** kwa kila vizazi hai **100,000** kwa mwaka 2023/2024 kufika vifo **123** kwa kila vizazi hai **100,000** (Zanzibar Vision 2050) na kufikia vifo **70** kwa kila vizazi hai **100,000** (SDG-2030) ifikapo 2030.

h. Kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka vifo **28** kwa kila vizazi hai **1,000** na kufikia vifo **26** kwa kila vizazi hai 1000 (Zanzibar Vision 2050) na hadi kufikia vifo **12** kwa kila vizazi hai **1,000** (SDG-2030) ifikapo 2030;

i. Kuimarisha uwezo na utayari wa kukabiliana na majanga ya mripuko na matukio mengine ya kiafya;

j. Kuendeleza mapambano ya maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza; na

k. Kuongeza idadi ya tafiti za afya kwa kuzingatia ajenda za nchi na kufanya uchambuzi wa tafiti hizo kwa lengo kutunga sera na miongozo ili kuimarisha huduma.

## MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

9. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mapato, Wizara ya Afya fungu (H01) ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 3,719,683,000**. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imepangiwa kukusanya **TZS 2,823,041,420.** Hadi kufikia Machi 2025, Wizara ilikusanya **TZS 3,756,153,554** sawa na asilimia **133** ya fedha zilizokadiriwa.

10. **Mheshimiwa Spika,** Hospitali ya Mnazi Mmoja fungu (H02) ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 1,339,086,000**. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Hospitali ya Mnazi Mmoja imepangiwa kukusanya **TZS 1,004,314,500.** Hadi kufikia Machi 2025 jumla **TZS 396,897,783** sawa na asilimia **40** zimekusanywa.

11. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya **TZS 282,756,472,000** zilikadiriwa kupitia fungu (H01) ambapo **TZS 71,599,300,000** ni kwa ajili ya mishahara, **TZS 74,056,499,000** kwa matumizi mengineyo, **TZS 7,992,300,000** ni ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara na **TZS 129,108,374,000** kwa kazi za maendeleo kati ya hizo **TZS 73,000,000,000** kutoka serikalini na **TZS 56,108,374,000** (**TZS 16,546,880,000** ruzuku na **TZS 39,561,494,000** mkopo) kutoka kwa washirika wa maendeleo.

12. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja Fungu (H02) imekadiriwa kutumia **TZS 61,329,600,000** kati ya hizo **TZS 10,702,060,000** ni kwa Programu ndogo ya Uchunguzi na Matibabu ( **TZS 4,900,000,000** kwa huduma za uchunguzi na **TZS 5,802,060,000** kwa huduma za matibabu). Aidha, **TZS 50,627,540,000** ni fedha za Programu ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ambapo (**TZS 23,069,600,000** kwa ajili ya mishahara, **TZS 4,558,940,000** kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa hospitali) na **TZS 23,000,000,000** (**TZS 21,000,000,000** Mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na **TZS 2,000,000,000** ni Mchango wa SMZ) kwa ajili ya Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

13. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya **TZS 212,067,354,750** zilipangwa kutumika kupitia fungu (H01), kati ya hizo **TZS 53,699,475,000** ni kwa ajili ya mishahara, **TZS 55,542,374,250** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS 5,994,225,000** kwa ajili ya ruzuku na **TZS 96,831,280,500** kwa kazi za maendeleo, kati ya hizo **TZS 54,750,000,000** kutoka serikalini na **TZS 42,081,280,500 (TZS 12,410,160,000** ni ruzuku na **TZS 29,671,120,500** ni mkopo) kutoka kwa washirika wa maendeleo.

14. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya **TZS 166,109,519,550** sawa na asilimia **78** zilitumika**.** Kati ya fedha hizo, **TZS 50,564,444,328** sawa na asilimia **94** zilitumika kwa mishahara na **TZS 55,119,806,616** sawa na asilimia **99** zimetumika kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS 5,701,095,554** sawa na asilimia **95** zimetumika kwa ajili ya ruzuku. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TZS 54,724,173,052** sawa asilimia **57** zimepatikana ambapo **TZS 32,801,424,954** sawa na asilimia **60** kutoka serikalini na **TZS 15,263,315,873** sawa na asilimia **123** kutoka kwa washirika wa maendeleo na **TZS 6,659,432,225** sawa na asilimia **22** ikiwa ni mkopo. **Kiambatisho Nambari 1a, 1b, 1c na 1d vinafafanua zaidi.**

**UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA**

**PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101)**

15. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kinga na kuongeza uelewa wa jamii juu ya njia mbali mbali za kujikinga na maradhi yakiwemo ya kuambukiza na yasiyoambukiza. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu hii ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS 100,619,301,000** kati ya hizo **TZS 24,661,259,000** kwa ajili ya mishahara na **TZS 11,901,718,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS 64,056,324,000 (TZS 38,525,000,000** kutoka serikalini na **TZS 25,531,324,000** kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya miradi ya maendeleo). Aidha, kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu hii

ilipangiwa jumla ya **TZS 75,464,475,750** kati ya fedha hizo **TZS 18,495,944,250** ni kwa ajili ya Mishahara, **TZS 8,926,288,500** kwa kazi za kawaida na **TZS 48,042,243,000** (TZS 28,893,750,000 kutoka serikalini na TZS 19,148,493,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo) kwa ajili ya kazi za maendeleo.

16. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya **TZS 63,236,628,508** sawa na asilimia **84** zimepatikana na kutumika. Kati ya fedha hizo **TZS 16,790,670,786** sawa na asilimia **91** kwa ajili ya mishahara, **TZS 3,617,006,754** sawa na asilimia **41** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS 42,828,950,968** (TZS 20,906,202,869 kutoka Serikalini, na **TZS 21,922,748,098** sawa na asilimia **114** kutoka kwa washirika wa maendeleo (TZS 15,263,315,873 kutoka kwa washirika wa Maendeleo na TZS 6,738,333,000,000 ni mkopo). Shughuli zifuatazo zilipangwa na kutekelezwa:
    a. Kuendelea kudhibiti maambukizi ya VVU kwa kutoa huduma za ushauri nasaha, upimaji na matibabu;
    b. Kuendelea kutoa huduma za tiba kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu, Ukoma na Homa ya Ini;
    c. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto;
    d. Kuimarisha huduma za afya ya Mipakani (Bandarini na Viwanja vya ndege);
    e. Kuendelea kutoa huduma za uchunguzi na tiba kwa maradhi ya macho katika vituo vya afya ya msingi, hospitali, skuli na jamii;

f. Kuendelea na mikakati ya kupambana na maradhi yanayoambukiza na yasiyoambukiza katika vituo vya afya ya msingi, hospitali, skuli na jamii;
g. Kuimarisha afya ya jamii na mazingira;
h. Kuendelea kufanya tafiti mbali mbali zitakazotoa matokeo ili kuimarisha huduma za afya katika kupambana na maradhi;
i. Kuimarisha programu za uhamasishaji na kutoa elimu ya afya katika ngazi zote; na
j. Kupambana na maradhi ya mripuko na majanga ya kiafya.

**HUDUMA ZA MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI, HOMA YA INI, KIFUA KIKUU NA UKOMA**

17. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2024/25, imekadiriwa kutujia jumla ya fedha **TZS 4,445,656,000** (TZS 380,000,000 kutoka Serikalini na TZS 4,065,656,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Aidha, Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2025, Jumla ya **TZS 3,334,242,000** zimetengwa ambapo **TZS 285,000,000** kutoka Serikalini na **TZS 3,049,242,000** kutoka kwa washirika wa maendeleo.

18. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufika Machi 2025 jumla ya **TZS 2,907,850,000** (TZS 37,850,000 kutoka Serikalini na TZS 2,870,000,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia **87** ya fedha zote zimeingizwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa.

19. **Mheshimiwa Spika**, Katika kupambana na maambukizi ya VVU Wizara imedhamiria kutokomeza ugonjwa huu ifikapo 2030. Hadi kufikia machi 2025 jumla ya watu **129,741** (57,615 Wanaume na 72,126 Wanawake) walipatiwa huduma za ushauri nasaha na uchunguzi wa VVU, kati ya hao **827** sawa na asilimia **0.6** waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU ambapo watu **775** Unguja (267 Wanaume na 508 Wanawake) na Pemba **52** (22 wanaume na 30 wanawake). Huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU kwa mwaka 2024/25 umepanda ukilinganishwa na upimaji wa VVU kwa mwaka 2023/24 ambapo jumla ya watu **65,643** walipimwa VVU, kati ya hao, watu **572** (187 wanaume na 385 wanawake) waligundulika na maambukizi ya VVU sawa na asilimia **0.8**. **Kiambatisho Nambari 2a kinafafanua.**

20. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, jumla ya kinamama wajawazito **55,416** walihudhuria kliniki wakati wa ujauzito, kati ya hao, **54,913** walipimwa VVU sawa na asilimia **99** ikilinganishwa na asilimia **90** ya upimaji wa VVU kwa mwaka 2023/24. Aidha, jumla ya wajawazito **82** waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU ambapo wajawazito wote waliweza kuunganishwa katika kliniki za huduma na tiba kwa wanaoishi na VVU pamoja na kuanzishiwa dawa za kupunguza makali ya VVU ili kumkinga mtoto dhidi ya maambukizi ya VVU.

21. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya watoto **351** waliozaliwa na mama wanaoishi na VVU wamepimwa VVU kwa kutumia mashine ya DNA-PCR ambapo jumla ya watoto **5**

waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU sawa na asilimia **1.4** ikilinganishwa watoto waliopimwa mwaka 2023/2024 ambapo watoto **347** walipimwa VVU na **6** kugundulika na maambukizi ya VVU sawa na asilimia **1.7**.

22. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa huduma mjumuisho za kuzuia maambukizi ya Kaswende na Virusi vya Homa ya Ini "B" kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Kwa kipindi cha julai hadi machi 2025, Jumla ya wajawazito **55,416** walihudhuria Kliniki kati ya hao **55,124** wamepimwa kaswende sawa na asilimia **99** kati ya mama hao **46** waligundulika kuwa na maambukizi na wote wamepatiwa matibabu ya Kaswende ikilinganishwa na wajawazito **24,101** waliopimwa kati ya **51,480** waliohudhuria kliniki sawa na asilimia **47** kwa mwaka 2023/24.

23. **Mheshimiwa Spika,** Katika kupambana na maambukizi ya homa ya Ini B jumla ya wajawazito **15,947** wamepimwa kipimo cha Homa ya Ini B, na mama **168** sawa na asilimia **0.3** walikutwa na maambukizi na tayari wameunganishwa kwenye huduma za matibabu ya homa ya ini B ikilinganishwa na mwaka 2023/2024 ambapo wajawazito **19,922** waliopimwa kati ya **51,480** waliohudhuria kliniki ambapo wajawazito **108** waligundulika na maambukizi ya Homa ya Ini "B" sawa na asilimia **0.5** kwa mwaka 2023/24.

24. **Mheshimiwa Spika,** Katika hatua nyengine, wizara inaendelea na kupambana na maambukizi ya homa ya Ini B na C katika jamii ambapo jumla ya watu **28,195** (18,095

wanaume na 10,100 wanawake) walipimwa virusi vya homa ya Ini B. Kati ya hao, watu **654** (439 wanaume na 215 wanawake) sawa na asilimia **2.3** wamegundulika kuwa na maambukizi. Aidha, Jumla ya watu wapya wenye maambukizi ya virusi vya homa ya Ini B **270** (110 wanaume na 160 wanawake) wamesajiliwa katika kliniki za homa za Ini (151 Unguja na 119 Pemba).

25. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa huduma ya homa ya Ini C, jumla ya watu **25,714** (16,842 wanaume na 8,872 wanawake) walipimwa virusi vya homa ya Ini C na watu **121** (89 wanaume na 32 wanawake) sawa na asilimia **0.4** wamegundilika kuwa na maambukizi ya virusi vya homa ya Ini C ikilinganishwa na mwaka 2023/2024 ambapo idadi ya wagonjwa waliogundulika walikuwa **184** (152 wanaume na 32 wanawake) kati ya watu **18,014** waliopimwa. **Kiambatisho Nambari 2b kinafafanua.**

26. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025 Jumla ya wateja **9,757** (3,012 wanaume na 6,745 wanawake) wanaoishi na VVU wanaendelea kupatiwa huduma kwenye kliniki **15** (11 Unguja na 4 Pemba) za huduma na tiba kwa wanaoishi na VVU. Kati ya wateja **9,757** wateja **9,529** (2,942 wanaume na 6,587 wanawake) sawa na asilimia **98.5** wanatumia dawa za kupunguza makali ya VVU (ARVs). Aidha, kwa kipindi Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya wateja wapya wanaoishi na VVU waliosajiliwa ni **785** (503 wanaume na 282 wanawake).

27. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wagonjwa **1,046** waligundulika na maradhi ya kifua kikuu (746 Unguja na 300 Pemba). Miongoni mwa wagonjwa hao watoto walikuwa **86** sawa na asilimia **8** na wagonjwa **39** walikuwa wanaishi na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI sawa na asilimia **3.7**, wagonjwa **3** kutoka Unguja waligundulika kuwa na kifua kikuu sugu. Aidha, waliogundulika wote wameanzishiwa matibabu ya Kifua kikuu.

28. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya wagonjwa **60** (52 Unguja na 8 Pemba) waligundulika na Ukoma ikilinganishwa na wagonjwa **50** (44 Unguja na 6 Pemba) kwa mwaka 2023/24. Wagonjwa wote waliogundulika wameanzishiwa matibabu ya Ukoma.

29. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya wagonjwa **22,493** (4,522 wanaume na 17,971 wanawake) wamegundulika kuwa na dalili na ishara za maradhi ya kujamiiana na wote wamepatiwa matibabu. Idadi ya wagonjwa imeongezeka ukilinganisha na mwaka 2023/2024 ambapo jumla ya wagonjwa **2,918** (618 wanaume na 2,300 wanawake) wamegundulika na kupatiwa matibabu. Ongozeko hilo limetokana na kuimarika kwa huduma za matibabu katika vituo vya afya sambamba na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa afya ili waweze kuibua visa vya maradhi ya kujamiana na kuwapatia matibabu kwenye vituo vyote vya afya Unguja na Pemba. **Kiambatisho Nambari 2c kinafanua zaidi.**

30. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwezi Machi 2025, jumla ya wateja **1,798** (1,713 wanaume na 85 wanawake) wameendelea kutumia dawa kwenye kituo cha huduma ya "Methadone" katika Hospitali ya Kidongo Chekundu Unguja. Aidha, kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wateja wapya **12** wamesajiliwa na kujiunga na huduma.

**HUDUMA ZA KUMALIZA MALARIA ZANZIBAR**

31. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya **TZS 7,931,393,000** (TZS 645,000,000 kutoka Serikalini na TZS 7,286,393,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Aidha, Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2025, Jumla ya **TZS 5,948,544,750** zimetengwa (TZS 483,750,000 kutoka Serikalini na TZS 5,464,794,750 kutoka kwa washirika wa maendeleo).

32. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya **TZS 4,775,332,848** sawa na asilimia **87** kutoka kwa washirika wa maendeleo zimetumika**.** Aidha, Programu ilipokea fedha ya ziada **TZS 4,159,000,883** kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya ununuzi wa vipimo vya malaria (mRDTs) na dawa za kupuliza za kuua mbu majumbani.

33. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024/2025 jumla ya washukiwa **522,304** (403,408 Unguja na 114,179 Pemba) wamechunguzwa vimelea vya malaria ambapo wagonjwa **9,652** (7,142 wanaume na 2,510 wanawake) sawa na asilimia **1.8** wamegundulika kuwa na vimelea vya malaria, visa **9,025** vimegundulika Unguja na **627** Pemba. Hali ya

maambukizi ya ugonjwa wa Malaria imepungua ikilinganishwa na mwaka 2023/2024 ambapo jumla ya washukiwa wa Malaria **442,939** (392,042 Unguja na 50,897 Pemba) walichunguzwa ambapo wagonjwa **19,579** sawa na asilimia **4.42** waligundulika kuwa na vimelea (19,074 Unguja na 505 Pemba) **Kiambatisho Nambari 2d Kinafafanua**.

34. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya wagonjwa **467** (438 Unguja na 29 Pemba) kati ya hao **311** wanaume na **156** wanawake wamepata malaria kali na kulazwa katika hospitali. Aidha, jumla ya vifo **5** vilitokana na malaria vimeripotiwa ikilinganishwa na vifo **29** mwaka 2023/24. Wilaya ya Mjini imeongoza kwa asilimia **24** ikifuatiwa na Magharibi B asilimia **22.** Takwimu zimeonesha kuwa waathirika wakubwa ni wanaume wenye umri kati ya miaka 15-35 kutoka kwenye makundi ya Wanafunzi, Walinzi, Wajenzi, Watembeza watalii, Waendesha bodaboda na Baba lishe.

35. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kupiga dawa katika maeneo yanayotoa wagonjwa wengi wa malaria na kutoa elimu juu ya kinga ili kumaliza ugonjwa wa malaria katika Wilaya zote **11**. Jumla ya nyumba **6,907** (5,276 Unguja na 1,631 Pemba) kati ya nyumba **7,440** sawa na asilimia **93** ya nyumba zilipigwa dawa ya kuuwa mbu wa malaria. Aidha, Jumla ya vyandarua **99,939** (68,824 Unguja na 31,115 Pemba) vilitolewa kwa wajawazito na watoto chini ya mwaka mmoja kupitia vituo vya afya ukilinganisha na mwaka 2023/24 ambapo vyandarua **93,225** (62,265 Unguja na 30,960 Pemba).

36. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuchukua fursa hii kutoa msisitizo kwa wananchi kuchukua tahadhari katika maeneo yao ili kujikinga na ugonjwa wa Malaria; ***"Jikinge na Malaria Kuimarisha Uchumi Wetu".***

## HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI, MAMA NA MTOTO

37. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/25 jumla ya **TZS 6,194,831,000** (TZS 1,000,000,000 kutoka Serikalini na TZS 5,194,831,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo) zimekadiriwa. Aidha, Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2025, Jumla ya **TZS 4,646,123,250** zimetengwa ambapo **TZS 750,000,000** kutoka Serikalini na **TZS 3,896,123,250** kutoka kwa washirika wa maendeleo.

38. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025, Programu imeingiziwa jumla ya **TZS 1,363,197,000** sawa na asilimia **42** kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya kutekeleza shughuli za huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto.

39. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wajawazito **44,351** wamejifungua kati ya hao **37,085** walijifungua katika hospitali na vituo vya afya. Aidha, wajawazito **5,309** walijifungua kwa njia ya upasuaji na wajawazito **1,957** wamejifungulia nyumbani. Wajawazito wote hao walipatiwa huduma ndani ya masaa **48** baada ya kujifungua.

40. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya vifo **40** vya kina mama vitokanavyo na uzazi viliripotiwa, Idadi hii imeshuka ikilinganishwa na vifo **60** vilivyoripotiwa mwaka 2023/2024. Aidha, jumla vifo **1,353** vya watoto wachanga vimeripotiwa ikilinganishwa na vifo **1,418** vilivyoripotiwa mwaka 2023/2024. **Kiambatisho Nambari 2e kinafafanua.**

41. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na jitihada za serikali katika kupunguza vifo vya mama na watoto wachanga, wizara inaendelea kutekeleza mfumo wa huduma za rufaa kwa mama wajawazito na watoto wachanga (M-Mama). Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya mama **724** (519 Unguja na 205 Pemba) na Watoto wachanga **69** (60 Unguja na 9 Pemba), walipatiwa huduma ya rufaa.

42. **Mheshimiwa spika,** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wateja wapya **27,440** (19,240 Unguja na 8,200 Pemba) walijiunga na njia mbali mbali za uzazi wa mpangilio ukilinganisha na wateja **27,035** (20,190 Unguja na 6,845 Pemba) mwaka 2023/24.

43. **Mheshimiwa Spika,** huduma za chanjo kwa makundi yote ziliendelea kutolewa ambapo jumla ya watoto **61,930** (41,519 Unguja na 20,411 Pemba) walipatiwa dozi ya tatu ya chanjo ya PENTA 3. Aidha, jumla ya wasichana **10,696** walipatiwa dozi ya chanjo ya kukinga saratani ya shingo ya

kizazi (HPV2). Katika hatua nyengine jumla ya akinamama wajawazito **61,446** walipatiwa chanjo ya pili hadi ya tano ya kinga dhidi ya pepopunda ili kumkinga mtoto mchanga mara tu baada ya kuzaliwa hadi kipindi cha mwezi mmoja. **Kiambatisho Nambari 2f kinafafanua zaidi**.

44. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha huduma za lishe jumla ya watoto **246,156** wenye umri wa miezi 6-59 wamepatiwa huduma za virutubisho vya vitamin A na upimaji wa hali ya lishe sawa na asilimia **94** ya watoto waliotarajiwa kupatiwa huduma hiyo kati ya watoto **261,156**.

## HUDUMA ZA MARADHI YASIYOAMBUKIZA

45. **Mheshimiwa Spika**, katika kupambana na maradhi yasiyoambukiza, wizara imeimarisha huduma za uchunguzi, matibabu na kutoa elimu ya afya kwa jamii. Jumla ya akinamama **5,811** wamechunguzwa saratani ya shingo ya kizazi kwa mwaka 2024/2025, ambapo **162** waligundulika na saratani katika hatua za awali (pre-cancerous lesion) na akinamama **27** waligunduliwa wakiwa na hatua za mwisho za saratani ya shingo ya kizazi (late stages). Takwimu zinaonesha kuongezeka kwa maradhi hayo ambapo kwa mwaka 2023/24, jumla ya akinamama **105** waligundulika na saratani ya shingo ya kizazi. Hivyo ni vyema kutoa elimu kwa jamii ili kuweza kufanya uchunguzi na kugundulika mapema kwani saratani inatibika endapo itagundulika katika hatua ya awali.

46. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya watu **4,724** wamepatiwa elimu na kuchunguzwa kisukari, shinikizo la damu na hali ya uwiano wa uzito na urefu (BMI) ambapo watu **299** wamegunduliwa kuwa ni wagonjwa wapya wa shinikizo la damu na watu **55** wamegunduliwa kuwa ni wagonjwa wapya wa kisukari, wagojwa wote wanaendelea kupatiwa matibabu kupitia hospitali na vituo vya afya mbali mbali Unguja na Pemba.

47. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya wagonjwa wa ajali za barabarani **1,224** (1,145 Unguja na 79 Pemba) zimeripotiwa katika hospitali na vituo vya afya kwa Unguja na Pemba. Aidha, jumla ya wagonjwa wa kiharusi **95** (79 Unguja na 16 Pemba) wameripotiwa na kupatiwa huduma stahiki kupitia kliniki za maradhi hayo.

**HUDUMA YA UFUATILIAJI WA MIENENDO YA MARADHI**

48. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya inaendelea kufuatilia kwa karibu mienendo ya maradhi na kuchukua hatua stahiki katika kuilinda jamii na maradhi mbali mbali yakiwemo ya miripuko. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya visa **134,158** vya maradhi viliripotiwa kutoka vituo vya afya na hospitali ikiwemo visa vya maradhi ya kuharisha, homa ya mapafu, tetekuanga na utapiamlo kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano.

49. **Mheshimiwa Spika,**Takwimu zinaonesha kuwa ugonjwa wa kuharisha bado unaongoza kuripotiwa kwa kuwa na visa **80,776** sawa na asilimia **60** ya visa vya maradhi ikifuatiwa na homa ya mapafu na vikohozi yenye visa **33,627** sawa na asilimia **25**, tetekuwanga (Chicken pox) visa **9,040** sawa na asilimia **7**, utapiamlo kwa watoto **1,867** sawa na asilimia **1** na homa ya matumbo (Typhoid) visa **847** sawa na asilimia **1**.

## HUDUMA ZA MARADHI YASIYOPEWA KIPAUMBELE

50. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya watu **1,683** (1,178 Unguja na 505 Pemba) walichunguzwa maradhi ya kichocho katika hospitali na vituo vya afya na kupatiwa matibabu ambapo watu **141** (120 Unguja na 21 Pemba) waligundulika kuwa na maradhi ya kichocho. Aidha, jumla ya watu **11,552** (6,126 Unguja na 5,426 Pemba) waligundulika kuwa na maradhi ya minyoo ya tumbo. Vile vile, wagonjwa **139** (106 Unguja na 33 Pemba) waligundulika na mabusha na wagonjwa **202** (155 Unguja na 47 Pemba) waligundulikwa kuwa na vimelea vya ugonjwa wa matende. Aidha, jumla ya wagonjwa **54** walifanyiwa upasuaji wa mabusha katika hospitali ya Kitogani na Vituo vya Afya Makunduchi na Kizimkazi.

51. **Mheshimiwa Spika,** wizara inaendelea kupambana na maradhi yasiopewa kipaumbele ambapo tathmini ya kuangalia ukubwa wa maradhi ya kichocho na minyoo imefanyika. Jumla ya shehia **199** (115 Unguja na 84 Pemba) zimeshiriki.

Matokeo ya tathmini yameonyesha kuwa hali ya maambukizi ya kichocho ni sawa na asilimia **1.6** kwa Unguja na asilimia **3.4** kwa Pemba. Aidha, kwa upande wa maambukizi ya minyoo ya tumbo matokeo yameonyesha asilimia **39.7** kwa Unguja na asilimia **83.4** kwa Pemba.

52. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea na zoezi la ulishaji wa dawa kinga kwenye jamii na skuli ili kupambana na maradhi haya. Jumla ya watu **1,317,698** sawa na asilimia **73.0** kwa dawa za kichocho, **1,485,211** sawa na asilimia **73.2** kwa dawa za minyoo na **1,489,289** sawa na asilimia **64.8** kwa dawa za matende/mabusha. Sambamba na hilo, wizara inaendelea kutoa elimu ya kujikinga na maradhi hayo.

## HUDUMA ZA MSINGI ZA MATIBABU YA MACHO

53. **Mheshimiwa Spika,** Katika kukabiliana na matatizo ya macho kwa jamii hasa vijijini, Wizara ilifanya uchunguzi wa macho kwa watu **6,480** (2,418 wanaume na 4,062 wanawake) katika maeneo tofauti Unguja na Pemba. Jumla ya wagojwa **44** (16 wanaume na 28 wanawake) walipewa rufaa ya kuendelea na matibabu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya Wete na Vitongoji. Aidha, jumla ya wagonjwa **28** (12 wanaume na 16 wanawake) waliweza kufanyiwa uchunguzi wa maradhi nyemelezi ya macho yanayosabishwa na matatizo ya Kisukari.

## HUDUMA YA UTOAJI WA ELIMU YA AFYA NA URATIBU WA WAHUDUMU WA AFYA NGAZI YA JAMII

54. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya watu **585,888** (222,632 Wanaume na 363,256 Wanawake) wamefikiwa na kupewa elimu ya afya ya kujikinga na magonjwa ya miripuko yakiwemo M-Pox, Ebola, Murbug  na magonjwa ya maambukizo kama vile Malaria, UKIMWI, Kifua Kikuu, Kipindupindu, athari za kiafya zinazotokana na udhalilishaji na unyanyasaji wa watoto, Usafi wa Mazingira, Uchangiaji Damu, Matumizi ya dawa za kutibu maji, Maradhi yasiyoambukiza, Uzazi wa mpangilio, Makuzi na malezi, Saratani, lishe, afya ya akili na chanjo mbalimbali.

55. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeweza kutoa elimu ya afya katika Vyuo, na Skuli ambapo jumla ya Skuli **536** (345 Unguja na 191 Pemba) na wanafunzi **354,357** (123,241 Wanaume na 231,116 Wanawake) wameweza kufikiwa ukilinganishwa na skuli **336** na wanafunzi **54,357** waliofikiwa kwa mwaka 2023/24. **Kiambatisho Nambari 2g kinafafanua zaidi.**

56. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya vipindi vya Redio **334** na vipindi **165** vya Televisheni vimerushwa. Vilevile, vipindi **399** viliandaliwa kuhusu afya ya akili ambavyo vimelenga madrasa, vikundi maalumu kwenye jamii, wanafunzi wa sekondari na vyuo, ambapo jumla ya washiriki **7,525** wamenufaika na elimu iliyotolewa. Aidha, elimu imeendelea kutolewa kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii, sambamba na hilo STUDIO

maalumu ya kurikodi na kuandaa vipindi vya elimu ya afya imeanzishwa ambapo zaidi ya vipindi **270** vimeandaliwa na kurushwa kupitia Online-TV.

57. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya wananchi **12,200** wamepiga simu kuripoti na kuuliza masuala mbalimbali ya kiafya na kupatiwa majibu kwa wakati kupitia kituo maalumu cha kuripoti na kupokea habari za magonjwa ya miripuko na dharura (AFYA CALL CENTER) chenye uwezo wa kuisaidia jamii kuripoti magojwa ya miripuko pale yanapotokea na kuchukua hatua stahiki. Aidha, kituo kimeimarishwa kwa kuweka mfumo maalum unaotumia "GPS" kwa ajili ya ufuatiliaji wa gari za dharura zinazotoa huduma za usafirishaji wa dharura kwa mama wajawazito na watoto wachanga kutoka kwenye jamii kupitia mfumo wa M-mama ambapo jumla ya gari **27** (20 Unguja na 7 Pemba) za kubeba wagonjwa zimefungwa mfumo huo.

## HUDUMA ZA AFYA NGAZI YA JAMII

58. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 jumla **TZS 6,689,750,000** (**TZS 1,500,000,000** kutoka Serikalini na **TZS 5,189,750,000** kutoka kwa washirika wa maendeleo) zilikadriwa kutumika. Kwa kipindi cha Julai hadi machi 2025, jumla ya **TZS 5,017,312,500** zimepangwa kutumika kati ya hizo **TZS 1,125,000,000** kutoka Serikalini na **TZS 3,892,312,500** kutoka kwa washirika wa maendeleo.

59. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia machi 2025, jumla ya **TZS 2,618,958,202.69** zimeingizwa sawa na asilimia **52.1** (TZS 560,173,060 kutoka Serikalini na TZS 2,058,785,142 kutoka kwa washirika wa maendeleo) kwa ajili ya kutekeleza shughuli za huduma za afya ya jamii.

60. **Mheshmiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii (CHW) **1,242** (903 Unguja na 339 Pemba) wamehitimu mafunzo yao ya miezi **6** kupitia vyuo mbali mbali vya afya hapa Zanzibar. Vile vile Wizara inaendelea kusomesha Wahudumu wa Afya wa kujitolea (CHV) **1,334** waliobakia katika vyuo vilivyochaguliwa kupitia mafunzo maalumu ya Miezi **6** ili kuendelea kuimarisha huduma za afya ngazi ya jamii.

**HUDUMA ZA AFYA YA MAZINGIRA**

61. **Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kuhakikisha kuwa jamii inatumia maji safi na salama imegawa vidonge **3,171,284** vya dawa za kutibu maji katika shehia **150** kwa lengo la kupunguza maradhi yatokanayo na maji yasiyo safi na salama.

62. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya sampuli **178** za maji ya kunywa zimechunguzwa kutoka katika vyanzo tofauti vya maji ambapo matokeo ya sampuli hizo zimeonyesha sampuli **97** sawa na asilimia **55** zina vimelea vinavyoweza kusababisha maradhi ya kuharisha na kutapika na sampuli **81** zimegundulika kuwa salama sawa na asilimia **46.** Hatua

za kuwapatia elimu wahusika katika vyanzo hivyo vya maji juu ya utaratibu wa kutibu maji zilichukuliwa pamoja na kuwapatia vidonge vya kutibu maji hayo.

63. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya maeneo ya biashara **126** yalikaguliwa ikiwemo mikahawa **25**, mamantilie **40**, wauza juice ya miwa **5**, wauza urojo **5**, wauza chipsi **15**, mikahawa midogo midogo mitano (**5**) na ukaguzi wa makaazi (**31**). Matokeo ya ukaguzi huo yalibaini kuwa maeneo yote yaliokaguliwa yanaonekana kuwa na changamoto za kutokufuata kanuni na miongozo ya kutolea huduma.

64. **Mheshimiwa Spika**, katika eneo la usimamizi na udhibiti wa taka zitokanazo na huduma za Afya katika vituo vya afya na hospitali za Serikali na binafsi, jumla ya tani **219.5** zimekusanywa na kuangamizwa katika tanuri la taka lililopo Kibele Unguja na kwa upande wa Pemba jumla ya tani **19.4** zimekusanywa na kuangamizwa katika tanuri la taka lililopo Vitongoji Pemba.

## HUDUMA ZA AFYA MIPAKANI (BANDARINI NA VIWANJA VYA NDEGE)

65. **Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi wa vyombo vya usafiri wa anga na baharini pamoja na abiria ulifanyika, ambapo jumla ya vyombo **22,776** vilikaguliwa, kati ya hivyo **16,795** ni vya anga na **5,981** vya usafiri wa baharini. Vyombo **11** vya baharini vilibainika kuwa na mapungufu ya kiafya na hatua zilichukuliwa kwa kutoa elimu ya afya na kupiga dawa.

66. **Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi wa abiria kupitia vyombo vya usafiri ulifanyika ambapo jumla ya abiria walioingia nchini na kukaguliwa ni **2,778,484** kati ya hao **2,209,099** walikuwa wenyeji na **569,385** walikuwa ni wageni, ambapo wasafiri **101** walibainika kuwa na nyuzi joto zaidi **37** walipofanyiwa uchunguzi wa awali, kati ya hao wasafiri **25** waligunduliwa kuwa na Malaria na kupatiwa huduma stahiki.

67. **Mheshimiwa Spika,** Chanjo kwa wasafiri zimeendelea kutolewa ambapo jumla ya dozi **6,066** zimetolewa, kati ya hizo, dozi **4,178** ni za homa ya manjano, dozi **1,647 ni** za homa ya uti wa mgongo na dozi **2,644** za homa ya Ini B na dozi ya polio **550**. Aidha, ukaguzi wa wagonjwa na maiti ulifanyika ambapo jumla ya wagonjwa **1,119** na maiti **269** walikaguliwa kupitia bandarini na viwanja vya ndege. Hakukua na maiti iliobainika kuwa na dalili za magonjwa ya kuambukiza.

## HUDUMA YA AFYA YA WAFANYAKAZI

68. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inahakikisha wafanyakazi kwenye Taasisi za Umma na Binafsi wanatoa huduma wakiwa na afya bora kazini. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya wafanyakazi **38,158** (35,091 Unguja na 3,067 Pemba) walichunguzwa afya zao kati yao wafanyakazi **1,171** ( 777 Unguja na 394 Pemba) walibainika kuwa na matatizo mbali mbali ya kiafya yakiwemo maambukizi ya mkojo, shinikizo la damu, uoni hafifu, Pumu, Kisukari na Maradhi ya ngozi. Wagonjwa wote waliobainika kuwa na matatizo walipatiwa huduma stahiki.

## HUDUMA ZA AFYA YA MSINGI YA AKILI

69. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeimarisha huduma za afya ya msingi ya akili kwa kuongeza vituo vinavyotoa huduma za afya ya akili kutoka **34** kwa mwaka 2023/2024 na kufikia vituo **55** (32 Unguja na 23 Pemba) kwa mwaka 2024/2025. Aidha, kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya watu **276,973** wamechunguzwa na kupatiwa matibabu ya nje (Outpatients) na wagonjwa **1,940** (1,472 wanaume na 468 wanawake) wamelazwa katika hospitali ya wagojwa wa akili Kidongo Chekundu kwa matatizo mbali mbali ya afya ya akili ikiwemo mpasuko wa mawazo (schizophrenia), Watumiaji wa madawa sugu (drug induced psychosis) na Sonona (depression).

70. **Mheshimiwa Spika,** Maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili Duniani yalifanyika kwa shughuli mbali mbali zikiwemo utoaji wa elimu ya afya ya akili katika jamii, skuli na hospitali ya wagonjwa wa akili Kidongo Chekundu. Jumla ya wananchi **314** walifikiwa huduma na elimu ya afya ya akili. Sambamba na hilo, Wizara imendelea kuwajengea uwezo wataalamu wa afya **24** kwa ajili ya kutibu magonjwa ya afya ya akili.

## UTEKELEZAJI WA BODI NA MABARAZA YA TAALUMA ZA AFYA

### BARAZA LA TAALUMA ZA AFYA YA JAMII NA MAZINGIRA

**71. Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Baraza limeweza kusimamia taaluma za kada ya Afya ya Jamii na Mazingira kwa kutoa usajili na leseni za kazi kwa Maofisa wa Afya ya Jamii na Mazingira. Baraza limesajili Maafisa Afya wapya **68** sawa na aslimia **91** ya lengo la kusajili maafisa afya **75.** Aidha, jumla ya Maafisa Afya **273** wamehuisha leseni zao sawa na asilimia **73** ya lengo la kuhuisha leseni kwa maafisa afya **375** kwa ngazi mbali mbali za shahada ya uzamili, shahada ya kwanza na stashahada.

### PROGRAMU YA HUDUMA ZA TIBA (PH0102)

**72. Mheshimiwa Spika,** Progamu hii ina jukumu la kuhakikisha jamii inapata huduma bora za tiba katika hospitali za wilaya na mikoa. Utekelezaji wa shughuli za Programu hii umegawika katika program mbili ndogo ya Huduma za Matibabu na Huduma za Uchunguzi.

**73. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu hii ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS 142,253,383,000** kati ya hizo **TZS 17,101,310,000** kwa ajili ya mishahara **TZS 54,647,823,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS 5,922,200,000** Ruzuku na **TZS 64,522,050,000** (TZS 33,945,000,000 kutoka serikalini na TZS 30,577,050,000 mkopo kutoka kwa washirika wa

maendeleo) kwa ajili ya kazi za maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu hii ilitengewa jumla ya **TZS 106,690,037,250** kati ya fedha hizo **TZS 12,825,982,500** ni kwa ajili ya mishahara na **TZS 41,008,367,250** kwa kazi za kawaida, **TZS 4,441,650,000** Ruzuku, **TZS 48,391,537,500** (TZS 25,458,750,000 kutoka serikalini na **TZS** 22,932,787,500 ni mkopo kutoka kwa washirika wa maendeleo).

**74. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya **TZS 75,768,008,994** sawa na asilimia **71** zimetumika. Kati ya hizo **TZS 11,382,626,034** mishahara sawa na asilimia **89**, **TZS 48,309,269,527** sawa na asilimia **118** kwa ajili ya matumizi ya kawaida, **TZS 4,180,891,348** sawa na asilimia **94** kwa ajili ya Ruzuku na **TZS 11,895,222,085** kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na asilimia **47** kutoka serikalini**.** Shughuli zifuatazo zilipangwa na kutekelezwa:

a. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za matibabu katika hospitali za wilaya na mkoa;
b. Kutekeleza mfumo wa rufaa kwa wagonjwa katika ngazi zote za utoaji wa huduma;
c. Kuimarisha kambi za matibabu na mashirikiano ya huduma za afya kimataifa;
d. Kuongeza ukusanyaji wa damu kutoka uniti **20,000** mpaka uniti **25,000** kwa mwaka;
e. Kuhakikisha upatikanaji wa Dawa, Vifaa, tiba na vitendanishi;
f. Kuimarisha huduma za uchunguzi (maabara na rediolojia);

g. Kuimarisha miundombinu ya afya katika ngazi zote za utoaji wa huduma za Afya;
h. Kuimarisha usimamizi katika uhifadhi na utumiaji wa dawa na vifaa vya utibabu katika hospitali na vituo vya afya;
i. Kuimarisha utoaji wa huduma kwa wahanga wa udhalilishaji;
j. Kuimarisha uratibu wa huduma za uuguzi na ukunga; na
k. Kuimarisha huduma za tiba kwa mashirikiano na sekta binafsi.

**PROGRAM NDOGO YA HUDUMA ZA MATIBABU**

75. **Mheshimiwa Spika,** Huduma za matibabu ya Wagonjwa wa nje na waliolazwa zinaendelea kutolewa katika hospitali za Mkoa, Wilaya, Hospitali Maalumu na za Binafsi. Jumla ya Mahudhurio ya wagonjwa wa nje ni **910,758** (346,762 wanaume na 563,996 wanawake), na wagonjwa waliolazwa ni **30,717** (13,023 wanaume na 17,694 Wanawake) **.** Aidha, wagonjwa **927** (451 wanaume na 456 wanawake) wamefariki dunia. Sababu kuu ya vifo hivyo ni pamoja na kiharusi, ubongo kukosa hewa wakati wa kuzaliwa watoto, upungufu mkubwa wa damu, homa kali ya mapafu kwa watoto, moyo kushindwa kufanya kazi na figo kushindwa kufanya kazi. Jumla wagonjwa **145** (115 Hospitali ya Lumumba na 30 Hospitali ya Abdulla Mzee) wanaendelea kupata huduma ya kusafisha damu "Dialiysis". **Kiambatisho Nambari 3a kinafafanua.**

## HUDUMA ZA UCHUNGUZI

**76. Mheshimiwa Spika,** Huduma za uchunguzi ni huduma zinazojumuisha uchunguzi wa maradhi kwa kutumia sampuli za aina mbalimbali zinazotokana na binaadamu. Uchunguzi hufanyika kwa njia picha (Radiology and Imaging Services) zikiwemo X-ray, Ultrasound, CT scan na MRI. Huduma hizi hutolewa katika hospitali za serikali na zile za binafsi. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imefanikiwa kupima vipimo **787,568** kwa wagonjwa. Kati ya hivyo maabara ni **651,866** (444,729 Unguja na 207,137 Pemba), kwa njia ya picha **135,702** (103,514 Unguja na 32,188 Pemba) kipimo kinachoongoza kwenye maabara ni vipimo vya kemia ambapo kipimo kwa njia ya picha ni Ultra-Sound ikifuatiwa na X Ray. Vipimo hivyo vimefanyika katika Hospitali zote za Unguja na Pemba. **Kiambatisho Nambari 3b kinafafanua.**

## HUDUMA ZA USHIRIKIANO WA AFYA KIMATAIFA

**77. Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi machi 2025, Wizara ya Afya imefanya kambi za uchunguzi na matibabu ya magonjwa ambapo jumla ya kambi **22** zimefanyika na wagonjwa **12,050** walipatiwa matibabu ya maradhi mbali mbali yakiwemo magonjwa ya akina Mama, moyo, matibabu ya macho, upasuaji wa jumla, mfumo wa mkojo na uchunguzi wa saratani.

78. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya wagonjwa **470** wamesafirishwa nje ya Zanzibar kwa matibabu zaidi ambapo Taasisi ya Mifupa ya Hospitali ya Taifa (MOI) **59**, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili **104**, Taasisi ya magojwa ya moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) **96** na Ocean Road **75**, India MIOT International Hospital **83** na KCMC **50**. **Kiambatisho Nambari 3c kinafafanua**

## HUDUMA ZA DAMU SALAMA

79. **Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imefanikiwa kukusanya jumla ya uniti **13,117** (9,541 Unguja na 3,576 Pemba) za damu kutoka kwa wachangiaji **14,174** sawa na asilimia **81** ambapo lengo lilikuwa ni kukusanya uniti **16,250**. Aidha, Jumla ya uniti za damu **13,505** sawa na asilimia **40** kati ya maombi ya uniti **33,288** zilisambazwa katika hospitali za Umma na Binafsi. Ukusanyaji huu ulifanikishwa kupitia uhamasishaji kwenye jamii kwa kurusha vipindi kupitia Redio na TV pamoja na mabonanza ya uchangiaji damu yaliyofanyika katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba.

## HUDUMA ZA MKONO KWA MKONO (ONE STOP CENTRE)

80. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Huduma kwa wahanga wa matukio ya udhalilishaji zimeendelewa kutolewa katika hospitali kupitia vituo vya

mkono kwa mkono. Jumla ya matukio **1,769** yameripotiwa yakiwemo jaribio la kubakwa **393**, kubakwa na kulawitiwa **335**, jaribio la kulawitiwa **34**, kulawitiwa **133**, kukashifiwa **147**, udhalilishaji kimwili **52**, udhalilishaji kijinsia **585**, na ujauzito **90. Kiambatisho Nambari 3d kinafafanua.**

## HUDUMA ZA BODI NA MABARAZA YA TAALUMA ZA AFYA

## BODI YA USHAURI YA HOSPITALI BINAFSI

**81. Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya maombi **40** ya vituo binafsi yaliwasilishwa; maombi **38** yalikuwa ya vituo vipya, maombi **2** yalikuwa ya vituo vinavyoomba kupandishwa daraja. Aidha, vituo **13** sawa na asilimia **34** vilikidhi vigezo vya kusajiliwa, vituo **18** sawa na asilimia **47** vilikuwa na mapungufu mbalimbali yaliyohitaji kuboreshwa na vituo **7** sawa na asilimia **18** havikukidhi vigezo.

**82. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya vituo na hospitali binafsi **73** zilikaguliwa katika Wilaya mbali mbali za Unguja zikiwemo Dispensari **56**, Vituo vya afya **2,** Polyclinic **13** na kliniki **2**. Kati ya hizo, Dispensari **2** zilifungwa kutokana na makosa mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhaba mkubwa wa wafanyakazi, miundombinu chakavu, ukosefu wa vifaa tiba, mazingira hatarishi ya kutolea huduma na kutozingatia miongozo ya kukinga na kuzuia maambukizi.

## BARAZA LA TIBA ASILI NA TIBA MBADALA

83. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala limepanga kusajili maeneo **36** ya tiba asili na tiba mbadala. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya maeneo **72** (56 Unguja na 16 Pemba) yamesajiliwa ikiwemo maduka ya dawa asili **22**, kliniki **9** za tiba asili, waganga wa tiba asili **20** na wasaidizi waganga wa tiba asili **21**. Sambamba na hilo, jumla ya leseni **117** (107 Unguja na 10 Pemba) zimehuishwa ikiwemo maduka ya dawa asili **59,** kliniki za tiba asili na tiba mbadala **17,** waganga wa tiba asili **30** na wasaidizi waganga **11**.

84. **Mheshimiwa Spika,** Baraza limefanikiwa kufanya operesheni maalum kwenye misikiti **19**, masoko **5**, pamoja na maeneo **10** ya mikusanyiko yakiwemo maonesho. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi limefanikiwa kuwafungulia kesi ya kufanya shughuli za tiba asili bila kusajiliwa na kwenye maeneo yasiyo rasmi watuhumiwa **6** ambapo kesi zote zimesharipotiwa kwenye vyombo vya sheria.

85. **Mheshimiwa Spika,** Baraza lilipanga kukagua pamoja na operesheni maalumu kwa maeneo **360** hadi kufikia Machi 2025, jumla ya maeneo **306** (242 Unguja na 64 Pemba) sawa na asilimia **85** ya lengo yalikaguliwa. Jumla ya maduka **26** yalifungwa kwa muda kwa sababu ya kutosajiliwa na Baraza hadi walipokamilisha taratibu kwa mujibu wa sheria pamoja na kuwapa onyo kwa maandishi kupitia fomu za

ukaguzi. Vile vile, Kliniki **1** ya tiba asili ilifutiwa usajili wake kutokana na kitendo cha kufanya udanganyifu pamoja na kukiuka miiko ya maadili ya tiba asili kwa wananchi.

86. **Mheshimiwa Spika,** Baraza limetoa jumla ya ruhusa **69** za uingizaji na usafirishaji wa dawa asili ambapo ruhusa za uingizaji wa dawa asili nchini ni **28** na dawa hizo zilitoka nchini India na Uturuki, vile vile ruhusa za usafirishaji wa dawa asili kwenda nje ya nchi ni **41** ambapo dawa hizo zilisafirishwa kwenda nchini Uingereza, Marekani, Canada na Oman.

## BARAZA LA MADAKTARI

87. **Mheshimiwa Spika;** Baraza la Madaktari limeendelea na usajili wa madaktari wapya **472** wakiwemo; madaktari bingwa wazawa **37**, madaktari bingwa wageni **6**, madaktari wazawa (MD) **101**, madaktari wa kigeni (MD) **5**, madaktari wa meno wazawa **6**, Afisa tatibu kinywa na meno **26** na Afisa tabibu **291**. Aidha, jumla ya madaktari **1,843** walitakiwa kuhuwisha leseni zao ambapo madaktari **1,342** walihuwisha leseni zao sawa na asilimia **73.**

## BARAZA LA WAUGUZI NA UKUNGA

88. **Mheshimiwa Spika,** Baraza limesajili jumla ya Wauguzi **811** ambapo Wauguzi Wakunga wapya **398** sawa na asilimia **99.5** ya lengo la kusajili wauguzi wapya **400**. Aidha, jumla ya wauguzi **413** wamehuisha leseni zao sawa na asilimia **48.5** (wazawa 410 na wageni 3) kati ya lengo la kuhuisha

usajili wa wauguzi **850**. Baraza kwa kushirikiana na Baraza la Wauguzi na Wakunga la Tanzania Bara limewapatia mafunzo ya utarajali (Internship) kwa wahitimu wauguzi **48**.

89. **Mheshimiwa Spika,** Baraza limeweza kukamilisha kutengeneza Muongozo wa utowaji wa mtihani wa leseni kwa Wauguzi na Wakunga wanao maliza masomo yao katika vyuo vya Uuguzi na Ukunga na tayari muongozo huo umeshapitishwa kwa matumizi.

## BARAZA LA WATAALAMU WA MAABARA ZA TIBA

90. **Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Baraza la wataalamu wa maabara za tiba limeendelea kusajili wataalamu wa maabara **210** kati ya hao wataalamu **163** waliohitimu masomo ya stashahada na **47** ni miongoni mwa wafanyakazi ambao wameshaajiriwa na wataalamu **291** waliweza kuhuisha leseni zao. Baraza lina jumla ya wataalamu wa maabara tiba **819** ambao wameshasajiliwa.

## HUDUMA ZA UUGUZI NA UKUNGA

91. **Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Idara imefanikiwa kufanya "mafunzo ya awali ya Muuguzi kazini" kwa wauguzi na wakunga waajiriwa wapya **152** (102 Unguja na 50 Pemba). Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uelewa wa kazi wauguzi na wakunga ili kuweza kutoa huduma stahiki kwa kuokoa maisha ya jamii hususan kina mama na watoto.

92. **Mheshimiwa Spika;** Idara imefanya ukaguzi elekezi katika vituo vya Afya na Hospitali Unguja na Pemba ambapo jumla ya vituo vya Afya (**23**) na Hospitali **7** za Wilaya kwa Unguja zilifikiwa. Jumla ya vituo vya afya **18** na hospitali **3** za Wilaya zilitembelewa kwa upande wa Pemba kwa lengo la kufatilia utendaji kazi wa wauguzi na wakunga. Ukaguzi huo ulibaini uhaba wa wafanyakazi hususan wauguzi na wakunga.

## HUDUMA YA UPATIKANAJI, UHIFADHI, USAMBAZAJI WA DAWA NA VIFAA TIBA

## OFISI YA MFAMASIA MKUU WA SERIKALI

93. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya **TZS 18,592,054,000** zilikadiriwa kutumika kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya **TZS 13,944,040,500** zilitengwa kununua Dawa na Vifaa tiba kwa vituo vya afya. Hadi kufikia Machi 2025, Jumla ya **TZS 11,694,636,990** zimepatikana sawa na asilimia **84** kwa vituo vya afya kwa ajili ya ununuzi wa Dawa na Vifaa Tiba.

94. **Mheshimiwa Spika;** Katika kuimarisha huduma za upatikanaji wa dawa Wizara imeanzisha kitengo cha kufatilia na kusimamia uhakiki wa mfumo wa ubora dawa "Qualilty Management Systems" kwa ajili ya huduma za dawa. Aidha, kwa mwaka 2024/2025, Wizara ilifanikiwa kutengeneza na kupitia miongozo mbali mbali ambayo itasaidia kurahisisha utekelezaji.

## WAKALA WA BOHARI KUU YA DAWA

95. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya **TZS 499,063,000** zimekadiriwa kwa matumizi ya uendeshaji wa Ofisi. Aidha, Wakala wa Bohari kuu ya dawa ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 30,000,000** kutoka vyanzo vya mapato ya uuzaji wa hewa tiba. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025, Wakala ilitengewa jumla ya **TZS 374,297,250** kwa matumizi ya uendesahaji wa ofisi na ilipangiwa kukusanya **TZS 22,500,000** kutoka vyanzo vya mapato ya uuzaji wa hewa tiba.

96. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi 2025, Wakala imefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS 123,950,615** sawa na asilimia **551** ya makadirio na **TZS 129,186,600** sawa na asilimia **35** zimetumika kwa kazi za uendeshaji wa Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa. Aidha, jumla ya **TZS 6,083,153,695** zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa Dawa na Vifaa Tiba kwa vituo vya afya.

97. **Mheshimiwa Spika,** Wakala imefanya usambazaji wa bidhaa zenye thamani ya **TZS 10,165,176,279** (TZS 7,053,250,917 Unguja na TZS 3,111,925,362 Pemba) katika vituo vya afya vya msingi na Hospital za Wilaya. Aidha, jumla ya mitungi **20,206** ya hewa tiba yenye thamani ya **TZS 441,458,750** imezalishwa na kusambazwa ambapo mitungi **17,490** yenye thamani ya **TZS 383,323,750** imesambazwa Unguja na mitungi **2,716** yenye thamani ya **TZS 57,135,000** imesambazwa Pemba.

98. **Mheshimiwa Spika;** Jumla ya mikataba **20** ilitayarishwa na kusainiwa baina ya Wakala na Taasisi, Kampuni tofauti kwa ajili ya kufanikisha utendaji kazi wa Wakala ikiwemo uuzaji, ununuzi na usambazaji wa dawa na vifaa Tiba pamoja na ujenzi wa Ghala ya kuhifadhia dawa na vifaa tiba - Dunga Zuze.

## PROGARAMU NDOGO YA HUDUMA ZA UCHUNGUZI (SH030202)

## WAKALA WA CHAKULA DAWA NA VIPODOZI

99. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, wakala ilipanga kufanya uchunguzi wa sampuli **2,960** za chakula, dawa na vipodozi. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya sampuli **2,133** zimechunguzwa sawa na asilimia **72** ikiwemo chakula **1,726**, dawa **272**, vipodozi **81** na vifaa tiba **54**. Matokeo yameonesha kuwa sampuli **65** (chakula 45, dawa 9, Vipodozi 3 na vifaa tiba 8) hazikufikia viwango vilivyowekwa na havikufaa kwa matumizi ya binaadamu.

100. **Mheshimiwa Spika,** Wakala imefanya ukaguzi wa majengo **3,676** (2,660 Unguja na 1,016 Pemba) kati ya majengo **5,077** sawa na asilimia **72.4** ya shabaha, katika ukaguzi huo jumla ya maduka **53** yalifungwa yakiwemo ya dawa **48** (27 Unguja na 21 Pemba), vifaa tiba **3** na chakula **2** kwa upande wa unguja. Vile vile, jumla ya tani **234.58** zikiwemo za chakula **218.08** dawa **12.5** na vipodozi **4** ziliteketezwa baada ya kutokidhi vigezo vilivyowekwa.

101. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wakala ilipanga kusajili majengo **1,113** ya Biashara ya bidhaa za Chakula, Dawa, Vipodozi na Vifaa Tiba. Hadi kufikia machi 2025, jumla ya majengo **1,069** (1,025 Unguja na 44 Pemba) yamesajiliwa sawa na asilimia **96**. Vilevile, jumla ya bidhaa **72** zilisajiliwa zikiwemo chakula **61**, dawa **4**, na vifaa tiba **7**. Aidha Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi imefanikiwa kuwa Mwanachama wa jukwaa la udhibiti wa vifaa tiba duniani (IMDRF) kuanzia tarehe 13.03.2025.

**WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI**

102. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2025, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imepanga kufanya uchunguzi wa sampuli **3,000**. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya sampuli **2,582** zimechunguzwa sawa na asilimia **86** ya lengo. Katika uchunguzi wa sampuli hizo sampuli **2,154** ni za makosa ya jinai, sampuli **158** ni za kemikali na bidhaa zitokanazo na kemikali, na sampuli **270** ni za chakula na dawa. Aidha, katika kufanya uchunguzi wa sampuli, sampuli **2,484** zimekidhi viwango na sampuli **98** hazikukidhi viwango. Hatua zilizochukuliwa kwa sampuli ambazo hazikukidhi viwango ni kuwaelimisha wateja ili kuzifanya bidhaa zao ziwe na viwango.

103. **Mheshimiwa Spika,** Katika udhibiti wa kemikali Zanzibar, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2024/25 ilikadiria kutoa vibali **2,100.** Hadi kufikia Machi

2025 jumla ya vibali **3,019** sawa asilimia **144** vya ruhusa za uingizaji, usambazaji na utoaji wa kemikali na bidhaa zitokanazo na kemikali vimetolewa. Kati ya hivyo vibali **2,797** ni vibali vya uingizaji wa kemikali na bidhaa zitokanazo na kemikali, vibali **214** vya utoaji kemikali na bidhaa zitokanazo na kemikali, na vibali **8** ni vya usafirishaji wa kemikali.

**104. Mheshimiwa Spika,** Wakala imefanya ukaguzi wa maeneo **275** (266 Unguja na 9 Pemba) yanayohifadhi kemikali na kusajili maeneo **87** (80 Unguja na 7 Pemba) ya kuhifadhia kemikali na maeneo **134** yalihuisha usajili.

## PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0103)

**105. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Afya inajumuisha programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, Mipango, Sera na Utafiti na Uratibu wa Wizara ya Afya Pemba na Tafiti za afya**.** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu hii ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS 39,883,789,000** kati ya hizo **TZS 29,836,731,000** kwa ajili ya mishahara na **TZS 7,476,958,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS 2,070,100,000** kwa ajili ya Ruzuku na **TZS 500,000,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu hii ilipangiwa jumla ya **TZS 30,037,841,750** Kati ya fedha hizo **TZS 22,377,548,250** ni kwa ajili ya

Mishahara na **TZS 5,607,718,500** kwa kazi za kawaida, **TZS 1,552,575,000** kwa ajili ya ruzuku na **TZS 500,000,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**106. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya **TZS 27,104,482,050** sawa na asilimia **90** zimetumika kati ya hizo **TZS 23,436,553,760** sawa na asilimia **105** kwa ajili ya mishahara na **TZS 2,147,724,084** sawa na asilimia **38** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS 1,520,204,206** sawa na asilimia **98**. Shughuli zilizopangwa na kutekelezwa ni kama ifuatavyo:

a. Kupeleka masomoni madaktari na wafanyakazi wa kada nyengine za afya;

b. Kuendelea kufanya tafiti mbali mbali zikiwemo tafiti za mimea inayotumika kwa Tiba asili;

c. Kufanya vikao vya pamoja na washirika mbali mbali wa masuala ya Afya ili kutatua changamoto kwa nguvu ya pamoja;

d. Kufanya ufuatiliaji wa sera na miongozo ya utoaji huduma za afya;

e. Kufanya ufuatiliaji na tathmini katika ngazi zote za utoaji wa huduma; na

f. Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa takwimu za afya.

## PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI (SH010301)

**107. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha wa 2024/ 2025, programu hii ilikadiriwa kutumia kiasi cha **TZS 10,225,229,000** kati ya hizo **TZS 4,477,543,000** kwa ajili ya mishahara, **TZS 5,747,686,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida**.** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, programu ilitengewa jumla ya **TZS 7,646,421,750**. Kati ya fedha hizo **TZS 3,358,157,250** ni kwa ajili ya mishahara na **TZS 4,310,764,500** kwa kazi za kawaida.

**108. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufika Machi 2025 jumla ya **TZS 7,365,705,806** sawa na asilimia **96** zimepatikana ambapo **TZS 4,798,465,806** sawa na asilimia **143** zimetumika kwa ajili ya mshahara na **TZS 2,567,240,000** sawa na asilimia **60** kwa ajili ya matumizi mengineyo na kutekeleza shughuli zifuatazo:

a. Kupeleka masomoni Madaktari na wafanyakazi wa kada nyengine za afya;

b. Kuendelea kufanya tafiti mbali mbali zikiwemo tafiti za mimea inayotumika kwa Tiba asili;

c. Kufanya vikao vya pamoja na washirika mbali mbali wa masuala ya Afya ili kutatua changamoto kwa nguvu ya pamoja;

d. Kufanya ufuatiliaji wa sera na miongozo ya utoaji huduma za afya;

e. Kufanya ufuatiliaji na tathmini katika ngazi zote za utoaji wa huduma; na

f. Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa takwimu za afya.

## NGUVU KAZI YA SEKTA YA AFYA

**109. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara ina jumla ya wafanyakazi **8,282** (6,098 Unguja na 2,184 Pemba). Aidha, wizara imeajiri jumla ya wafanyakazi **1,075** (**629** Unguja na **446** Pemba) kwa fani tofauti ambao tayari wameshapangiwa kazi katika hospitali na vituo vya Afya Unguja na Pemba. **Kiambatisho Nambari 4a kinafafanua zaidi.**

**110. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha wafanyakazi wanapata stahiki zao, jumla ya wafanyakazi **37** wamelipwa fedha za ubani na wafanyakazi **89** wamepandishwa daraja. Aidha, wafanyakazi **25** wamestaafu kwa mujibu wa kanuni na sheria za Utumishi wa umma, wafanyakazi **7** wamechukua likizo bila ya malipo na wafanyakazi **2** wamefariki dunia, Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu peponi, Amin.

**111. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Jumla ya watumishi **268** wamepewa ruhusa ya kwenda masomoni katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi wakiwemo madaktari bingwa **23**, bobezi **2** na wauguzi bingwa **14**, wauguzi ngazi ya shahada ya kwanza

**32** na watumishi **167** wanaosomea kada nyengine za afya na kufanya idadi ya watumishi waliopo masomoni kufikia **924**. Aidha, hadi kufikia Machi 2025, jumla ya watumishi **67** wamerudi masomoni. **Kiambatisho Nambari 4b na 4c vinafafanua zaidi.**

## HUDUMA ZA UNUNUZI NA UONDOAJI WA MALI ZA UMMA

**112. Mheshimiwa Spika;** Wizara inaendelea kuratibu shughuli za Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ambapo kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya zabuni **6** vimejadiliwa zikiwemo ujenzi wa vituo vya afya ambavyo ni Mombasa na Welezo kwa Unguja na kwa upande wa Pemba Kiungoni. Aidha, Kitengo kimefanikiwa kutafuta mshauri elekezi kwa ajili ya kuandaa michoro na kusimamia ujenzi wa Hospitali ya Mkoa Kaskazini Unguja. Pia, Kitengo kimejadili zabuni ya kumtafuta mshauri elekezi kwa ajili ya kusimamia ujenzi wa Hospitali ya Rufaa na kufundishia Binguni (Hub Consultancy). Vilevile, Wizara imefanikiwa kununua generator la Maabara ya Afya ya Jamii Binguni. **Kiambatisho Nambari 4d Kinafafanua zaidi.**

## HUDUMA ZA AFYA KIDIGITALI

**113. Mheshimiwa Spika;** Wizara ya Afya katika kuimarisha utoaji wa huduma imefanya maboresho ya mfumo wa Zan-EMR kupitia Mradi wa Uwekezaji wa Afya ya Mama na Mtoto Tanzania kupitia mkopo wa Benki ya Dunia, ambapo hadi sasa mfumo huu umeanza matumizi katika Kituo cha Afya

Kizimkazi na unategemewa kuanza kutumika katika Vituo vyengine vya Afya. Zoezi la kuunganisha mifumo ya taarifa za afya linaendelea ambapo jumla ya mifumo **12** (Kadi ya Matibabu, SHAMS, NSK, Jamii ni Afya, e-LMIS, M-Mama, ZanEMR, Zan-ITN, Zan-LIS, MCN, MassITN, na IDSR) kwa sasa inasomana.

**114. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha na kuongeza matumizi ya TEHAMA**,** Wizara imenunua komputa **53** na routers **22** kwa ajili ya vituo vya afya vya msingi ili kuimarisha utoaji huduma ikiwemo huduma za Mfuko wa Huduma za Afya (ZHSF).

**115. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha huduma za kibingwa na bobezi zinapatikana katika hospitali, Wizara imeendelea kuimarisha Kitengo cha huduma za Tiba mtandao kwa kufungwa vifaa vya kisasa katika hospitali za Wilaya na Mkoa zikiwemo Lumumba na Abdulla Mzee. Kuimarishwa kwa huduma hizi kutasaidia kupunguza gharama za matibabu za kusafirisha wagonjwa nje ya nchi.

## PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI (SH010302)

**116. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la uandaaji wa mipango na bajeti ya sekta, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa kazi za wizara na programu za miradi ya maendeleo, kutayarisha na kuzifanyia mapitio Sera na Miongozo pamoja na kuratibu na kufanya tafiti za afya.

117. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/25 programu hii ilikadiriwa kutumia **TZS 2,093,456,000**, kati ya fedha hizo **TZS 1,015,842,000** kwa ajili ya mishahara, **TZS 577,614,000** matumizi mengineyo na **TZS 500,000,000** kwa kazi za maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu hii ilitengewa jumla ya **TZS 1,610,092,000** kati ya fedha hizo **TZS 734,192,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **TZS 375,900,000** kwa kazi za kawaida na **TZS 500,000,000** kwa kazi za maendeleo.

118. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufika Machi 2025 jumla ya **TZS 843,444,712** zimepatikana sawa na asilimia **52** kati ya hizo **TZS 690,935,109** sawa na asilimia **91** kwa ajili ya mishahara na **TZS 152,509,603** sawa na asilimia **35** kwa ajili ya matumizi mengineyo na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

119. **Mheshimiwa Spika**, Katika kuimarisha mashirikiano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo Wizara imefanya mkutano wa **14** wa mapitio na mpango wa pamoja wa sekta ya Afya ambao mkutano huu pia umewashirikisha taasisi zisizo za kiserikali na sekta binafsi. Kauli mbiu ya mkutano huu ilikuwa ni "**Uwepo kwa mfumo bora wa huduma za afya ya msingi uliounganishwa, bunifu, na unaojengwa kwa ushahidi ili kufikia lengo la upatikanaji wa Afya Jumuishi kwa Wote**".

**120. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya mafunzo ya uongozi na utawala kwa wakuu na wasaidizi **82** wa vituo vya afya kwa Unguja. Kuwajengea uwezo watendaji **40** (25 Unguja na 15 Pemba) kutoka Timu za Afya za Wilaya juu ya uandaaji wa maandiko ya Miradi. Sambamba na hilo, Wizara imeandaa Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati wa Kugharamia Huduma za Afya pamoja na muongozo wa usimamizi na matumizi ya fedha kwa ajili ya vituo vya afya ya msingi.

**121. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha mipango na kufanya maamuzi yenye ushahidi wa kitakwimu Wizara inaendelea kuandaa na kuchapisha jarida la kila mwaka la taarifa za afya (Zanzibar Annual Health Bulletin). Aidha, jumla ya maafisa **20** walipatiwa mafunzo ya uandishi wa mapendekezo ya tafiti kutoka Idara na Taasisi mbalimbali za Wizara ya Afya.

**122. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha ubora wa huduma za afya katika ngazi zote, Wizara imefanya mafunzo kwa wakufunzi (TOTs) na watoa huduma juu ya utoawaji wa huduma za utu na heshima (Respectful care and Effective Communication), ambapo jumla ya wakufunzi **6** (4 Unguja na 2 Pemba) na watoa huduma **350** (238 Unguja na 112 Pemba) walipatiwa mafunzo hayo. Aidha, jumla ya watumishi **15** walipatiwa mafunzo ya awali ya uongozi wa hospital (Basic Hospital Management).

**123. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya afya kwa kushirikiana Tanzania Health Summit imeweza kuandaa kongamano la **11** ambalo ni la kwanza kwa Zanzibar. Jumla ya washiriki **1,835** kutoka nchi **14** walihudhuria ambapo mada **196** ziliwasilishwa, mikutano ya kitaalamu **40** na maonesho **74** ya kitafiti yamefanyika. Katika kongamano hili, mafunzo ya taaluma za afya pamoja na uhamasishaji wa jamii juu ya matumizi ya huduma mbali mbali za afya yalitolewa.

## MIRADI YA MAENDELEO

**124. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/25 Wizara inaendelea kusimamia miradi ya maendeleo katika maeneo mbali mbali ya utoaji wa huduma za afya. Wizara imepanga kutekeleza programu **7** na miradi **2** ya maendeleo yenye thamani ya **TZS 129,108,374,000** (TZS 73,000,000,000 kutoka Serikalini na TZS 56,108,374,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya **TZS 96,831,280,500** zilipangwa kutumika. kati ya hizo **TZS 54,750,000,000** kutoka serikalini na **TZS 42,081,280,500** (TZS 12,410,160,500 ni msaada kutoka kwa wahisani na TZS 29,671,120,500 ni mkopo) kutoka kwa washirika wa maendeleo.

**125. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya **TZS 40,638,761,393** sawa asilimia **42** zimepatikana ambapo **TZS 20,641,666,062** sawa na asilimia **38** kutoka serikalini na **TZS 13,337,663,105** sawa na asilimia **107** kutoka kwa washirika wa maendeleo na **TZS 6,659,432,225** sawa na asilimia **22** ikiwa ni mkopo.

**126. Mheshimiwa Spika,** kati ya programu zinazotekelezwa na Wizara, programu ya ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika Hospitali za Wilaya na Mkoa umefikia asilimia **85** ambapo jumla ya **TZS 6,475,000,000** zimepangwa ambapo hadi kufikia Machi 2025, jumla **TZS 6,554,092,631** sawa na asilimia **101** zimetumika.

**127. Mheshimiwa Spika,** Programu ya ukarabati na ujenzi wa vituo vya afya ya msingi upo kwenye hatua nzuri ambapo jumla ya vituo **14** vinaendelea na ujenzi. Kwa mwaka wa fedha 2024/25, jumla ya **TZS 35,000,000,000** zimepangwa kutumika kwa Programu hii. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya **TZS 20,308,179,809.31** sawa na asilimia **58** zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa vituo ambavyo ni Mpendae (Magomeni Wandaras), Sebleni, Tumbatu, Nungwi, Tunguu, Mahonda (Kinduni), Welezo, Mtoni Basra, Rahaleo, Jadida, Konde, Chonga, Maziwa Ngo'mbe na Mtambile.

**128. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha miundombinu ya afya kwa mwaka wa fedha 2024/25 programu hii ilikadiriwa jumla ya **TZS 27,000,000,000.** Wizara inaendelea na Ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa ambapo ujenzi huu utagharimu **TZS 27,605,938,329**. Hadi kufikia Machi 2025 malipo ya awali ya mkandasi wa ujenzi yenye thamani ya **TZS 5,521,187,666** yamewasilishwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

129. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja (Mahonda) ambao kwa mwaka wa fedha 2024/2025 umetengewa jumla ya **TZS 15,000,000,000.** Hadi kufikia Machi 2025 Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja (Mahonda) umeanza kwa awamu ya kwanza chini ya ufadhili wa Serikali ya Oman na mradi umefikia asilimia **30** ambapo umehusisha jengo la mama na mtoto. Aidha, awamu ya pili ya ujenzi huu unatekelezwa kupitia fedha za Serikali ambapo jumla ya **TZS 3,750,000,000** zimetengwa kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2025. Jumla ya **TZS 179,172,154** zimeshaombwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ikiwa ni malipo ya mshauri elekezi kwa ajili ya kazi za kuandaa michoro na kufanya thamani ya ujenzi wa jengo (Bill of Quantity), kwa sasa hatua inayofuata ni kumuajiri Mkandarasi ili aanze kazi.

130. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa hospitali ya wagonjwa wa akili na nyumba za wafanyakazi Pandani katika Wilaya ya Wete unaendelea. Mradi huu unafadhiliwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (50%) na Haukeland University Hospital ya nchini Norway (50%). Gharama za ujenzi kwa mujibu wa mkataba ni **TZS 5,975,090,000**. Hadi kuifikia Machi 2025, jumla ya **TZS 1,035,832,198** zimelipwa kutoka SMZ na **TZS 1,522,003,912** zimelipwa kutoka Haukeland University Hospital.

**131. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Afya Pemba ambao kwa mwaka wa fedha 2024/25 ulitengewa jumla ya **TZS 1,250,000,000** kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2025, jumla **TZS 54,541,265** zimeshaombwa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa ajili ya malipo ya mshauri elekezi kwa kazi za kuandaa michoro na kufanya thamani ya ujenzi wa jengo (Bill of Quantity).

**132. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na hatua za utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa na Kufundishia Binguni. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Mradi huu umetengewa jumla ya **TZS 30,577,000,000** ambazo ni mkopo kutoka Korea Exim Bank. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2025 jumla ya **TZS 7,644,250,000** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. Hadi kufikia Machi 2025, Wizara inaendelea na hatua ya zabuni ya kumtafuta mshauri elekezi wa kufanya tathmini ya gharama za ujenzi (BOQ).

## MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR (ZHSF)

**133. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) ulikadiria kukusanya **TZS 48,240,000,000** kutoka katika vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Machi 2025 jumla ya **TZS 35,534,000,000** sawa na asilimia **74** zimekusanywa.

134. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko umefanya malipo kwa watoa huduma ambapo madai yenye thamani ya **TZS 6,104,948,911** yamelipwa sawa na asilimia **78** ya madai yaliyopokelewa yenye thamani ya **TZS 7,803,000,000**.

135. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko umefanya uwekezaji wa jumla ya **TZS 40,500,000,000** katika benki ya PBZ, NBC na SUKUK na kupata faida ya **TZS 2,111,000,000**. Mfuko umeendelea na zoezi la usajili kwa waajiri wapya **588** (541 Unguja na 47 Pemba) sawa na asilimia **168** ya lengo la kusajili waajiri **350**. Hadi kufikia Machi 2025 jumla ya wanachama **173,200** walikadiriwa kusajiliwa ambapo Mfuko ulifanikiwa kusajili jumla ya wanachama **113,970** (90,036 Unguja na 23,934 Pemba) sawa na asilimia **66** ya lengo lililowekwa. Wanachama hao wanajumuisha Sekta ya Umma **29,824** Binafsi **28,654** na Sekta isiyo rasmi **55,492**.

136. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko unaendelea kutoa elimu ya ushajihishaji kwa jamii, ambapo jumla ya mikutano **140** (72 Unguja na 68 Pemba) imefanyika. Aidha, machapisho **10,810** ya vifaa vya matangazo yametolewa, vipindi vya TV na Radio **26** vimerushwa. Vilevile, jumla ya mijumbe mifupi (sms) **156,342** imetolewa kwa Unguja na Pemba.

*** **Napenda kutoa wito kwa wananchi hususan sekta isiyo rasmi kujiunga na Mfuko wa Huduma za Afya ili kuwa na fedha endelevu za kugharama huduma za matibabu.**

## TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZA BINAADAMU (ZAHRI)

137. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Taasisi ya Utafiti wa Afya ilikadiriwa kutumia **TZS 2,070,100,000** kati ya hizo **TZS 1,492,300,000** kwa ajili ya mshahara na **TZS 577,800,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Taasisi ilitengewa jumla ya **TZS 1,552,575,000** Kati ya fedha hizo **TZS 1,119,225,000** kwa ajili ya mshahara na **TZS 461,020,305** kwa kazi za kawaida.

138. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025 jumla ya **TZS 1,520,204,206** sawa na asilimia **98** ziliingizwa, kati ya hizo **TZS 1,127,266,206** sawa na asilimia **101** kwa ajili ya mishahara na **TZS 392,938,000** sawa na asilimia **91** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, jumla ya **TZS 637,159,505** zimepatikana kutoka kwa Taasisi za Kitafiti za nje kwa ajili ya kufanya tafiti mbali mbali ikiwemo utafiti wa usugu wa dawa za antibiotiki kwa watoto chini ya umri wa miaka **13**.

139. **Mheshimiwa Spika,** Taasisi imeendelea na utafiti wa ongezeko la thamani kwa dawa za miti shamba “Phase 2” kwa ajili ya kutibu maradhi yasioambukiza Zanzibar. Jumla ya sampuli **4** za dawa zimeshatengenezwa ikiwemo dawa za kutibu presha, kisukari na pumu za vidonge na dawa za maji.

**140. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza jukumu la kuratibu, kudhibiti na kusimamia utekelezaji wa tafiti mbalimbali nchini, taasisi imefanya mapitio ya matoleo ya tafiti (Research Proposals) kwa ajili ya kutoa vibali kwa wadau wa afya na wanafunzi wanaotaka kufanya tafiti. Jumla ya matoleo ya tafiti **429** (385 kutoka kwa wanafunzi na 44 ni miradi). Matoleo yote yaliyopitiwa yalipitishwa na kupewa ruhusa ya kuendelea na tafiti zao.

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA WIZARA YA AFYA PEMBA (SH010303)**

**141. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025, programu hii ilikadiriwa kutumia kiasi cha **TZS 25,525,004,000** kati ya hizo **TZS 24,343,346,000** kwa ajili ya mishahara, **TZS 1,181,658,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida**.** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu ilitengewa jumla ya **TZS 19,143,753,000** Kati ya fedha hizo **TZS 18,257,509,500** ni kwa ajili ya mishahara na **TZS 886,243,500** kwa kazi za kawaida.

**142. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufika Machi 2025 jumla ya **TZS 17,375,127,325** sawa na asilimia **91** zimepatikana kati ya hizo **TZS 16,901,746,593** sawa na asilimia **93** zimetumika kwa ajili ya mishahara na **TZS 473,380,732** sawa na asilimia **53** kwa ajili ya matumizi mengineyo na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

**143. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya wafanyakazi **64** wamechukuwa likizo lao la kawaida kati ya hao, **20** wamelipwa stahiki zao za likizo, wafanyakazi **9** wa kada mbalimbali wamestaafu, na mfanyakazi **1** amechukua likizo bila malipo. Kwa upande mwengine mfanyakazi **1** amefariki dunia Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema Peponi, Amiin.

**144. Mheshimiwa Spika,** Kambi mbali mbali za matibabu zilifanyika katika hospitali ya Wilaya Micheweni na Vitongoji kwa magonjwa ya kina mama, macho, koo, pua na masikio (ENT) ambapo jumla ya wagonjwa **934** (526 Wanaume na 408 wanawake) walifanyiwa uchunguzi. Aidha, wagonjwa **392** (206 Wanaume na 186 wanawake) walifanyiwa upasuaji na wagonjwa **542** walipatiwa ushauri na matibabu katika hospitali ya Micheweni na Vitongoji.

**145. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya Pemba imefanikiwa kupata hati miliki **40** kati ya maeneo **85** ambapo maeneo **22** yako katika hatua za kupatiwa hatimiliki na **23** yako katika hatua za uhakiki ili kuanza taratibu za upimaji.

## PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (FUNGU H02)

**146. Mheshimiwa Spika,** Hospitali ya Mnazi Mmoja (H02) ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 1,339,086,000**. kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, na jumla **TZS 396,897,782.65** sawa na asilimia **29.6** zimekusanywa.

**147. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja Fungu (H02) imekadiriwa kutumia **TZS 61,329,600,000** kati ya hizo **TZS 10,702,060,000** sawa na asilimia **11** ni kwa Programu ya Uchunguzi na Matibabu (**TZS 4,900,000,000** kwa huduma za uchunguzi na **TZS 5,802,060,000** kwa huduma za matibabu). Aidha, **TZS 50,627,540,000** ni fedha za Programu ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ambapo **TZS 23,069,600,000** kwa ajili mishahara, **TZS 4,558,940,000** kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa hospitali. Kwa upande wa Mradi wa Maendeleo, jumla ya **TZS 23,000,000,000** (TZS 21,000,000,000 Mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 2,000,000,000 ni Mchango wa SMZ) kwa ajili ya Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

**148. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja Fungu (H02) imepangiwa kutumia **TZS 51,392,800,000** kati ya hizo **TZS 8,044,287,000** kwa ajili ya Programu ya uchunguzi na matibabu na **TZS 43,348,513,000** ni fedha za Programu ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ambapo **TZS 17,302,200,000** kwa ajili ya mshahara na **TZS 3,541,591,050** kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji. Aidha, **TZS 22,504,723,450** kwa ajili ya Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

**149. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025, Jumla ya **TZS 23,687,235,714** sawa na asilimia **46** ya bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 zimetumika. Kati ya fedha hizo **TZS 4,725,043,441** ni matumizi ya programu ndogo ya uchunguzi na matibabu na **TZS 18,962,192,272** (TZS 16,410,955,838 Mshahara na TZS 2,551,236,494 Uendeshaji) kwa matumizi ya Uendeshaji na Uratibu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

**150. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mradi wa Maendeleo jumla ya **TZS 346,174,400** zimeingizwa kwa ajili ya malipo ya mshauri elekezi na mishahara ya wafanyakazi wa Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kutoka kwa washirika wa maendeleo. Shughuli zilizotekelezwa kupitia programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ni kama ifuatavyo;

**151. Mheshimiwa Spika,** jumla ya vipimo vya maabara **252,987** na vipimo **29,576** kwa njia ya picha vilifanyika katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Aidha, jumla ya wagonjwa wa nje **194,804** walitibiwa (Wanaume **84,924 na** Wanawake **109,880**) na wagonjwa **8,133** (wanaume **3,978 na** wanawake **4,205**) walilazwa kwa magonjwa tofauti. Kwa upande wa Hospitali ya Kidongo Chekundu, jumla ya wagonjwa **851** (wanaume **586** wanawake **265)** walilazwa.

152. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya wajawazito **5,318** (Mwembeladu **1,203** na Mnazi Mmoja **4,115**) walipokelewa, kati ya hao wajawazito **1,850** walijifungua kwa njia ya kawaida katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na wajawazito **1,872** walijifungua kwa njia ya Upasuaji. Aidha, wajawazito **1,063** walijifungua kwa njia ya kawaida katika Hospitali ya Mwembeladu.

153. **Mheshimiwa Spika,** Kambi za uchunguzi na matibabu zimeendelea kufanyika kwa mashirikiano na Madaktari Bingwa kutoka Hispania, Uholanzi, Israel, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (JKCI na MOI) na Christian Blind Mission (CBM). Jumla ya kambi **10** zilifanyika na wagonjwa **499** walichunguzwa na kupatiwa matibabu. Kati ya hao, wagonjwa **390** (250 wanaume na 107 wanawake) na watoto **33** walifanyiwa upasuaji ikiwemo mishipa ya fahamu, macho na vichwa.

154. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya wanafunzi **1,800** wamepokelewa kwa ajili ya kufanya mazoezi ya vitendo chini ya usimamizi wa wataalamu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa mujibu wa fani zao. Aidha, vibali **20** vimetolewa kwa kufanya tafiti ndani ya hospitali na wafanyakazi **61** walipatiwa mafunzo tofauti ili kuwajenga uwezo katika kazi zao.

## C. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**155. Mheshimiwa Spika;** Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta ya afya, bado tunaendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo: -

1. Msongamano wa wagonjwa katika hospitali za Wilaya na Mkoa hususani kwenye wodi za wazazi hali inayopelekea malalamiko kwa wananchi kutokupatiwa huduma kwa wakati;
2. Kutokufikiwa kwa viwango vya ubora kitaifa na kimataifa katika utoaji wa huduma kwa vituo vya afya ambao inapelekea ugumu wa kutekelezwa kwa mfumo wa rufaa;
3. Uhaba wa wataalamu wenye sifa katika utoaji wa huduma za Kibingwa na Bobezi kama vile madaktari bingwa, wataalamu wa ganzi na usingizi, wataalamu wa ICU, wahandisi vifaa tiba, Wauguzi wenye shahada ya kwanza, Wakaguzi wa kemikali n.k;
4. Upungufu wa vifaa vya kutendea kazi kama vile PET scan, mashine ya kuchunguzia sumu (LCMS/MS), DR6000 spectrophotometry na MP-AES;
5. Miundombinu hafifu ya uendeshaji wa mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za wagonjwa (Electronic Medical Record (EMR) katika vituo vya afya vya msingi ikiwemo ukosefu wa huduma za intaneti na vifaa vya TEHAMA;
6. Upatikanaji wa fedha usioridhisha kwa ajili ya uendeshaji wa Wizara na utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

7. Kuongezeka kwa maradhi yasiyoambukiza yakiwemo maradhi ya shinikizo la damu na Kisukari;
8. Uchakavu wa miundombinu ya vituo vya afya ikiwemo majengo, mashine na vifaa tiba;
9. Kuongezeka kwa matumizi ya dawa za asili kutokana na uuzaji holela wa dawa za asili katika maeneo mbali mbali;
10. Lishe duni ya mama na mtoto inayopelekea maradhi na vifo vinavyotokana na uzazi kwa mama na watoto;
11. Wajawazito kuchelewa kuhudhuria kliniki; na
12. Kutopatikana kwa taarifa za afya kwa ukamilifu na kwa wakati kutoka katika vituo vya afya vya binafsi.

## HATUA ZA UTATUZI WA CHANGAMOTO

**156. Mheshimiwa Sipka;** Kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji majukumu hayo, Wizara imejipanga kutatua kama ifuatavyo:-

1. Kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali za Wilaya na Mkoa kwa kuwahamasisha wananchi kutumia mfumo wa rufaa, kuongeza kasi ya kumaliza ujenzi wa vituo vya Afya na Dispensari katika maeneo yanayotoka wagonjwa wengi na kuimarisha miundombinu na huduma katika baadhi ya vituo vya afya kwa kila Wilaya na kuviwezesha kutoa huduma kwa masaa 24 na siku za mapumziko;

2. Kuongeza wafanyakazi wa afya kwa kuajiri wataalam wenye ujuzi kupitia Serikali na Kampuni binafsi zinazoendesha hospitali za Wilaya na Mkoa;

3. Kuweka miundombinu na kufunga vifaa vya mtandao ili kuongeza kasi ya mtandao (internet) ambapo Wizara imeingia mkataba na Shirika la Simu TTCL kwa ajili ya kupeleka mkonga kwenye vituo vya afya **142**. Vile vile Shirika la UNICEF limeingia mkataba na Wizara kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya TEHAMA ikiwemo mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za wagonjwa ZanEMR;

4. Kuendelea kutekeleza mpango mkakati na endelevu wa kugharamia huduma za afya ikiwemo kutumia fursa zinazotolewa na mfuko wa huduma za afya (ZHSF) sambamba na kufungua akaunti za hesabu za vituo vya afya na hospitali;

5. Kuendelea kutoa elimu kwa jamii jinsi ya kuepuka vichocheo vya maradhi kuambukiza na yasiyoambukiza kwa kutumia vyombo vya habari na huduma mkoba (out reach services);

6. Kuwatumia wahudumu wa afya ngazi ya jamii kuwasajili, kuwachunguza, kuhamasisha wajawazito kuwahi kliniki na kujifungulia katika vituo vya afya; na

7. Kuwasiliana na wamiliki wa vituo vya afya na hospitali binafsi ili kuweza kuhakikisha wanaingiza taarifa za wagonjwa kwenye mfumo kwa kutumia fomu maalumu zilizoandaliwa na Wizara.

## D. MWELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

**157. Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 naomba sasa niwasilishe vipaumbele vya Wizara ya Afya na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kuanza na vipaumbele vya Wizara.

**158. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya kwa mwaka 2025/26 imeweza kutenga bilioni **22,522,840,000** sawa na asilimia **6** kwa ajili ya kuzingatia Usawa wa Kijinsia. Fedha hizo zitatumika pamoja na afua nyengine, kuongeza ushiriki wa wanaume katika masuala ya afya ya uzazi, kuimarisha huduma Rafiki kwa Vijana (YFS) na kuendelea kuhamasisha wanaume wenza kuambatana na wake zao kupima VVU wakati wa ujauzito.

**159. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Afya inaendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa miaka mitano 2020/21-2024/25 ambao kwa mwaka huu unamaliza muda wake wa utekelezaji. Hata hivyo Wizara imefanya mapitio ya Sera ya afya ya mwaka 2011. Rasimu ya Sera ya Afya ya Zanzibar ya mwaka 2025 inayopendekezwa imezingatia vipaumbele vyote muhimu ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals) 2015-2030, Agenda ya Afrika 2063, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 ya Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021-2026.

**160. Mheshimiwa Spika,** Kupitia rasimu hiyo Wizara imejipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo kulingana na maeneo makuu sita (Health Sector Six Building Blocks):-

## I. UTOAJI WA HUDUMA

- Kuimarisha Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto;
- Kuimarisha huduma za Afya ya Msingi (PHC) na Afya ya Jamii;
- Kuimarisha ufuatiliaji wa magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza;
- Kutekeleza mpango mkakati wa kisekta wa lishe wa mwaka 2024/2025 – 2028/2029;
- Kuimarisha huduma za msingi za afya ya akili; na
- Kuwekeza katika malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto kuanzia umri 0 mpaka miaka 8.

## II. RASILIMALI WATU KWA SEKTA YA AFYA

- Kuajiri na kutoa mafunzo kwa wataalamu wa afya;
- Kupanua wigo wa programu za mafunzo ya kujiendeleza kwa wauguzi, wakunga, na wataalamu wa kada nyengine za afya;
- Kuimarisha mfumo wa kidigitali wa kuhifadhi kumbukumbu za taarifa za wafanyakazi, na
